

**ARSENAL KUTOMWACHIA GABRIEL KUTUA MADRID**

UKURASA 21

**ULEVI**, ubakaji, ulawiti tatizo Kilimanjaro

UKURASA 9



**RC** alia vijana kutumia mikopo kucheza kamari

UKURASA 10



**GAMONDI:** Hakuna wa kumwogopa makundi

UKURASA 24

Jumatatu Septemba 23, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581808

www.ippmedia.com

LIKE & FOLLOW US

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

# Waiangukia CHADEMA

**NI** kuhusu maandamano yao, polisi watanda mikoa mitatu *Ukurasa wa 2*



"Ni maandano ya amani. Hatufurahii uvunjifu wowote wa sheria wala hatukusudii kuharibu amani ya nchi yetu..."

**FREEMAN MBOWE**



"Tunatoa wito pande zote kutuliza vichwa na kutoa nafasi kwa hekima na busara za uongozi zitumike kufanya ufumbuzi na suluhisho..."

**DOROTHY SEMU**



"Yeyote aliyealikwa, asithubutu kufanya hivyo kwani maandamano hayo ni haramu na hayatafanyika..."

**DCP DAVID MISIME**



Jeshi la Polisi Mkoa wa Simiyu likifanya mazoezi katika mitaa mbalimbali ya Mji wa Bariadi, mkoani Simiyu jana kwa lengo la kuimarisha usalama wa raia na mali zao. **PICHA: JESHI LA POLISI**

## Sanamu la Nyerere la kilo 6,000 labomolewa, vipande vyaibwa

UKURASA 4

## Wananchi Z'bar waingiwa hofu uamuzi serikali kubinafsisha kisiwa cha Kwale

UKURASA 17

**MICHEZO** SIMBA SC YATINGA MAKUNDI ILIPOZOEA UK. 24

**KATUNI** UK. 6

# ACT Wazalendo waiangukia CHADEMA

**Na Waandishi Wetu**

CHAMA cha ACT Wazalendo kimekiomba Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kusitisha maandamano ya amani yaliyopangwa kufanywa leo, kikizitaka pande zote kurudi nyuma na kuwa na mazungumzo zaidi.

Kukiwa na rai hiyo ya ACT, mitaani jana askari wa Jeshi la Polisi walitanda kuimarisha hali ya ulinzi na usalama mkoani Dar es Salaam, hali hiyo ikishuhudiwa pia katika mikoa ya Morogoro na Mkoa wa Kipolisi Tarime/Rorya.

CHADEMA imeshikilia msimamo wa kuendelea kuandamana kwa amani kuomboleza wenzao waliouawa na kushinikiza serikali kuchukua hatua kudhibiti mauaji na watu kutekwa.

Maandamano hayo yanalenga kuomboleza vifo vya viongozi wa chama hicho na matukio ya kutekwa, kuteswa na kuuawa kwa wananchi yaliyoripotiwa nchini hivi karibuni.

Pia yanalenga kuishinikiza serikali kufanyia kazi maagizo waliyoipa Septemba 11, mwaka huu, ikiwamo kuwataka Waziri wa Mambo ya Ndani, Hamad Masauni na viongozi waandamizi wa Jeshi la Polisi kujiuzulu.

Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Dorothy Semu, ameomba CHADEMA kuahirisha maandamano ya amani na badala yake serikali ichukue hatua ili kujenga nchi.

Dorothy alisema jana kuwa mvutano huo umepelekea kila upande unaohusika kukaza kamba na kutetea msimamo wake, hali ambayo aliitaja "haitoi nafasi ya vichwa kutulia na kutafuta suluhisho la kiuongozi litakalotutoa hapa".

"Tunatoa wito pande zote kutuliza vichwa na kutoa nafasi kwa hekima na busara za uongozi zitumike kufanya ufumbuzi na suluhisho mwafaka.

"Tanzania inayo hazina ya watu wenye busara na hekima wakiongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan na viongozi wetu wa dini ambao wakifanya kazi pamoja, wanaweza kututoa kwenye hali iliyopo sasa na tukatoka tukiwa imara zaidi kama taifa na hata kuwa mfano kwa wengine kama ilivyo historia yetu adhimu.

"Mimi binafsi (Dorothy Semu) na Mwenyekiti wa Chama Taifa, Othman Masoud Othman tunafanya mazungumzo na pande zote mbili katika jitihada za kupata mwafaka wa hali tuliyo nayo," alisema Semu.

Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe kupitia Twitter Space ya chama hicho jana, aliwakumbusha wananchi kuwa maandamano hayo yatafanyika leo kuanzia saa tatu asubuhi.

Alisema kuwa Septemba 11 mwaka huu, chama hicho kiliwataarifu Watanzania kuwa kitafanya maandamano hayo leo kama serikali haitoonesha mwanga wa kushughulikia maagizo walioyatoa kwayo, ikiwa ni sehemu ya kutafuta wanachokiita "suluhu ya matukio ya utekaji, utesaji, ya mauaji ya Watanzania wasio na hatia".

Alisema ndani ya miezi mitatu, viongozi sita wa chama hicho walitekwa katika mazingira yanayoashiria kuhusika kwa vyombo vya ulinzi na kuzua taharuki kwa wananchi.

Mbowe alisema taharuki iliongezeka baada ya kutekwa kwa Mjumbe wa Sekretarieti ya chama hicho taifa, Ally Kibao, Septemba 7 mwaka huu kisha kuuawa na mwili wake kukutwa ukiwa umetupwa eneo la Ununio, Tegeta, Dar es Salaam Septemba 8 mwaka huu, ukiwa na majeraha.

Alisema baada ya tukio hilo chama hicho kilizungumza na vyombo vya habari na kuwataka Waziri wa Mambo ya Ndani, Masauni na viongozi waandamizi wa Jeshi la Polisi kama sehemu muhimu ya uwajibikaji.

Mbowe alisema pia waliagiza kurejeshwa viongozi wao waliotekwa kwa zaidi ya mwezi mmoja, wakiwa hai au wamefariki dunia, wakiwamo Katibu Mwenezi wa Sumbawanga Mjini, Dionise Kipanya, Katibu wa Chama Wilaya ya Temeke, Jacob Mlay na Katibu Mwenezi, Muheza mkoani Tanga, Mbwana Kombo.

Alisema pia waliitaka serikali kuruhusu uchunguzi huru utakaofanywa na wachunguzi huru kutoka Scotland Yard kwa madai kuwa vyombo vya usalama nchini ni sehemu ya watuhumiwa wa matukio hayo, hivyo haviwezi kujichunguza.



Alisema kufuatia vitendo hivyo, chama hicho kilikubaliana kutangaza mwezi wa maombolezo, bendera zao zikipepea nusu mlingoti huku wakisubiri hadi Septemba 21, kama hakutokuwa na hatua zozote za kutoa mwanga kutoka serikalini, watafanya maandamano ya maombolezo jijini Dar es Salaam leo.

Alisema kuwa hadi Septemba 21, hakuna agizo lolote walilolitoa lililopewa nafasi ya kufanyiwa kazi na serikali au kujibiwa badala yake, wameona idadi kubwa wa askari wenye silaha kali wakiletwa Dar es Salaam wakiwa na silaha na magari ya aina mbalimbali, yakiwamo yenye maji ya kuwasha, farasi, mbwa, mabomu.

Mbowe alisema kwa mujibu wa sheria, waliiandikia barua polisi kuwaleza nia ya kufanya maandamano ya amani na maombolezo leo, lakini walitoa katazo badala ya ulinzi huku viongozi wao wakiendelea kukamatwa na kufunguliwa mashtaka.

Mboye aliwasisitiza Watanzania kuwa maandamano hayo ni ya maombolezo na amani yasiyolenga kupambana na mtu yeyote wala kubeba silaha ya aina yoyote kwa lengo la kudhuru au kujeruhi mtu yeyote.

"Hatufurahii uvunjifu wowote wa sheria wala hatukusudii kuharibu amani ya nchi yetu kama inavyojaribu kuaminishwa na viongozi wa serikali," alisema Mbowe.

Alisema kuwa chama hicho kinafanya kazi zake kwa kuzingatia Katiba na sheria za nchi na kipo kwa mujibu wa Katiba ya nchi inayotoa haki ya kukusanyika na kujumuika.

Mbowe alirejelea pia Kifungu cha 11 (4) cha Sheria ya Vyama vya Siasa, kinatoa haki ya chama kufanya maandamano kwa kutoa taarifa kwa OCD, jambo ambalo walifanya.

Alisema ni matumaini ya chama hicho kuwa serikali na vyombo vyake vyote vitaheshimu haki yao ya kikatiba na sheria na kulinda maandamano yao ya amani na maombolezo badala ya kuyazuia na kuyatawanya kwa nguvu.

"Hatutegemei falsafa ya maridhiano igeuke kuwa mafarakano, falsafa ya ustahamilivu igeuzwe hasira na chuki, falsafa ya mageuzi igeuzwe ukiritimba wa chama kimoja na ujenzi mpya ugeuzwe uadui na umwagaji damu," alisema Mbowe.

Kaimu Mwenyekiti wa CHADEMA Bara, Tundu Lissu, alisema maandamano hayo si uhalifu na mara zote alizokuwa anakamatwa, hajawahi kutiwa hatiani.

Alisema amepata taarifa kuwa atakamatwa muda wowote kuanzia jana na kuwa amejiandaa kwa lolote na kuwa itakuwa ni mara ya pili kukamatwa na Jeshi la Polisi ndani ya miezi miwili, na mara ya 10 kukamatwa na Jeshi la Polisi ndani ya miaka minane, lakini alipona baada ya kupigwa risasi 16.

"Wakati wa uongozi wa (Benjamin) Mkapa nilikamatwa mara moja, wa (Jakaya) Kikwete mara tatu, wa (Dk. John) Magufuli mara nane. Hii itakuwa mara ya pili katika uongozi wa (Rais) Samia. Mara zote sijawahi kutiwa hatiani na mahakama yoyote, sijawahi kutenda kosa la jinai, mimi ni mpigania uhuru na haki", alidai.

Jana waandishi wa Nipashe walitembelea maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam na kukuta askari polisi wakiwa na magari yenye maji ya kuwasha. Baadhi ya maeneo hayo ni Kituo Kidogo cha Polisi Kitunda, eneo la JET karibu na uwanja wa ndege, Taraza katika Daraja la Mfugale, Buguruni, Shekilango na Mwenge.

Mkoa wa Kipolisi Tarime Rorya jana zaidi ya magari 10 yenye askari polisi wa Kikosi cha Kutuliza Ghasia (FFU), Kikosi cha Mbwa na maji ya kuwasha yalionekana yakifanya doria kwenye mitaa mbalimbali.

Vilevile, mkoani Morogoro, askari polisi walionekana kwenye mitaa mbalimbali wakifanya mazoezi ya kawaida ya utayari.

Katika Mkoa wa Kipolisi wa Tarime Rorya, askari hao wakiwa kwenye magari, walionekana majira ya asubuhi, wakizunguka katika wilaya zote sita za Sirari, mjini Tarime, Nyamwaga, Utegi Shirati na Kinesi.

Alipoulizwa kuhusu misafara hiyo, Kamanda wa Polisi Tarime Rorya, SACP Michael Njera, alisema hatua hiyo ni utaratibu wa jeshi hilo kuzungukia wilaya zao za kipolisi wakihimiza amani.

"Tunahimiza amani kwa taifa letu na kujiweka katika utayari kwa lolote linaloweza kutokea la uvunjivu wa amani. Tunawaasa wananchi kuwa na uzalendo na kutunza amani," alisema Kamanda Njera.

Pia aliwataka wananchi kushirikiana na jeshi hilo katika kuimarisha ulinzi wa taifa kwa kutoa taarifa za viashiria vya uvunjivu wa amani na uhalifu kwa kuwa ulinzi na amani kuwapo kunahitaji ushirikiano kati ya wananchi na Jeshi la Polisi.

Mkoani Morogoro, Kamanda wa Polisi Alex Mkama alisema mazoezi yanayofanyika ni ya utayari kwa kutumia magari, kutembea na kukimbia.

"Mazoezi hayo yamefanyika leo (jana) kupita maeneo ya FFU, Kichangani, Msamvu, Kihonda, Mazimbu, Madeko, Chamwino, Tumbaku, Mafiga, Kiwanja cha Ndege, Maskika, Sabasaba, Boma Road na stendi ya zamani," alisema.

Alisisitiza kuwa mazoezi hayo ni ya kawaida na hufanywa na askari kila mwisho wa wiki kwa ajili ya kujiweka sawa.

Septemba 13, mwaka huu, Jeshi la Polisi lilipiga marufuku kufanyika maandamano hayo ya CHADEMA, likitoa sababu kuwa ni kielelezo cha uvunjifu wa amani.

Akiwa mkoani Arusha siku hiyo, Msemaji wa Jeshi la Polisi, DCP David Misime, alisema maandamano hayo ni haramu na kutoa onyo kwa viongozi wa CHADEMA kuacha kuendelea kuwahamasisha wananchi kujihusisha kwa kuwa ni uhalifu.

"Jeshi la Polisi linatoa katazo kwa yeyote aliyealikwa, kuelekezwa kufika Dar es Salaam kutoka mkoa wowote ule kwa ajili ya maandamano hayo, asithubutu kufanya hivyo kwani maandamano hayo ni haramu na hayatafanyika," alionya DCP Misime.

***Imeandaliwa na Samsoni Chacha (TARIME), Halfani Chusi na Jenifer Gilla (DAR)***

JAKAYA KIKWETE CARDIAC INSTITUTE

medanta

hosplan

**JKCI and Hosplan welcome Dr Praveen Chandra**



**Dr. Praveen Chandra**
Chairman – Interventional Cardiology
Medanta - The Medicity, India

**"Welcome Dr. Praveen Chandra"**

Chairman – Interventional Cardiology
Medanta - The Medicity, India

Continuing Medical Education (CME) Session

**Advances in Coronary & Valvular Heart Intervention**

Organised by Jakaya Kikwete Cardiac Institute,
In Collaboration with Treatment Traveller Tanzania Limited

**Date: 24th September 2024**

**Interested Cardiac sciences-specialist doctor please contact on +255748555889 for participation**

HABARI KITAIFA



Baadhi ya wakazi wa Kijiji cha Suguti wilaya ya Musoma mkoani Mara, wakiangalia moja ya nyumba zilizoezuliwa na mvua ilionyesha usiku wa kuamkia jana, ikiambatana na upepo mkali. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Machifu wampongeza Rais Samia kuthamini utamaduni

**Na Elizabeth Zaya**

VIONGOZI wa kimila kutoka mikoa mbalimbali nchini, wamempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuanzisha Tamasha la Utamaduni la Kitaifa pamoja na kuongeza thamani ya viongozi wa mila iliyoonekana kushuka kwa miaka mingi. Wamesema hatua hiyo ya kuthamini, kufufua misingi na kuenzi tamaduni zilizokuwa zimeanza kuwekwa kando, itasaidia kwa kiwango kikubwa kulinda maadili na tamaduni za Kitanzania.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti mkoani Ruvuma linakofanyika Kongamano la Tatu la Utamaduni la Kitaifa, viongozi hao wa kimila walisema jana kuwa kwa miaka mingi mila na tamaduni za Kitanzania zilionekana kutokuthaminiwa, lakini Rais Samia ametambua umuhimu wake na kuzifufua.

"Tunamshukuru Chifu Hangaya (Rais Samia), yeye kama kiongozi namba moja wa machifu wote Tanzania, ameona umuhimu wa kuenzi mila na tamaduni zetu ambazo zilikuwa zimeachwa kupewa kipaumbele sana.

"Kwa ufupi ni kwamba amezifufua na kuupa thamani kubwa utamaduni wa Mtanzania, na kwa kuwa yeye ndiye msimamizi mkuu, tunaamini maadili ya nchi yetu yatalindwa zaidi," alisema Chifu Nyamironda, ambaye ni Katibu Mtendaji wa Umoja wa Machifu Tanzania.

"Leo hii viongozi wa kimila wanakaa pamoja, wanajadili mstakabali wa taifa lao, hili ni jambo jema sana na tunaamini hili litazidi kulinda pia utulivu na amani kwenye nchi yetu kwa sababu viongozi wa kimila wana nafasi na nguvu kubwa katika jamii zao wanazoongoza," aliongeza.

Belinje Yasini, Mwenyekiti wa Machifu Mkoa wa Dodoma, alisema kuwa kati ya tunu ya kujivunia ni kuwa Mtanzania na kwamba, umoja na mshikamano uliopo unapaswa kulindwa zaidi.

"Amani, umoja na mshikamano tulionao ni vya kulindwa sana kwa sababu kuna baadhi ya mataifa yanatamani kuwa kama sisi, lakini hayawezi.

"Sisi tunakaa pamoja, tunazungumza lugha moja, ni wakarimu, wenye upendo na utulivu licha ya kuwa tuna makabila mengi, lakini bado tunadumisha na kulinda umoja wetu tofauti na ilivyo kwa mataifa mengine," alisema Chifu Yasini.

"Yaani tungekuwa na ukabila, tukabaguana, tukatengana, tungeenda kuishi wapi? Lakini taifa teule, lililobarikiwa kuliko mataifa yote, tunamshukuru Mungu tumezidi kuwa na mshikamano na amani, ni vyema tukaendelea kulinda tunu hii ambayo tumepewa na Mwenyezi Mungu," alisema.

Chifu Yasini alisema kitendo cha Rais Samia kutambua mchango wa viongozi hao wa dini ni jambo jema na anapaswa kupongezwa na kuungwa mkono kutimiza azma yake ya kuhakikisha Tanzania inaendelea kulinda tamaduni na maadili yake.

"Tumekuwa na viongozi wengi waliopita katika nafasi hiyo ya Rais, lakini hawakuzipa nguvu kubwa tamaduni zetu kama ilivyo kwa Rais Samia, hivyo tunampongeza katika hili, tumuunge mkono ili kurejesha tamaduni zetu na kupambana na tamaduni potofu zisizo zetu ambazo zimeanza kuchangia mmomonyoko wa maadili katika taifa letu," alinsema Chifu Yasini. Aliongeza: "Tushirikiane na Rais Samia kupambana na vitendo vinavyochangia mmomonyoko wa maadili katika taifa letu, yeye ameonesha njia na sisi tufuate.

"Tunapoona leo kuna unyanyasaji, ukatili wa kijinsia na vitendo vingine vinavyotokea sasa, kazi ya kupambana navyo si ya serikali pekee, ni yetu sisi sote kama jamii."

Alisema viongozi wa mila wana mchango wa kipekee katika kujenga taifa lenye mshikamano, amani, utulivu na kuchangia katika maendeleo endelevu yanayozingatia urithi wa kitamaduni na maadili ya kitaifa.

Chifu Yasini alisema viongozi hao wa kimila wamekuwa hawashirikishwi kwenye mambo mengi kwa kutokuthamini umuhimu wao.

"Unakuta mtu anatoka mbali huko anakuja anakusanya watu kupiga kampeni, lakini kiongozi wa mila wa eneo husika hashirikishwi na ndio maana wakati mwingine baadaye huwa mambo yanakuja kutugharimu au kuharibika, hivyo thamani aliyoonesha Rais Samia kwa sasa kwa viongozi hawa, liwe funzo kwa wengine na ninaamini tutafika mbali," anasema Chifu Ismail Hassan kutoka Nachingwea, mkoani Lindi.

# Majaliwa atinga UN, ateta na Katibu Mkuu

**Na Mwandishi Wetu,**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amekutana na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Gutierres katika makao makuu ya umoja huo na kujadiliana masuala kadhaa, yakiwamo ya maendeleo ya jamii, ulinzi na usalama, siasa na ushirikiano wa Tanzania na UN.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya mkutano wao uliofanyika mwishoni mwa wiki, Waziri Mkuu ambaye yuko Marekani akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan kwenye Mkutano wa 79 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA79), alisema kuwa katika suala la maendeleo ya jamii, wamejadiliana umuhimu wa kuinua uwezo wa wananchi kiuchumi, ikiwamo upatikanaji huduma zote muhimu.

Kuhusu ulinzi na usalama, Waziri Mkuu alisema Tanzania imepongezwa kwa kusimamia ukombozi wa nchi nyingi za Afrika, hasa za ukanda wa Jumuiya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

"Sasa hivi serikali yetu inaendelea kuunga mkono kwa kupeleka vikosi vya ulinzi katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na za SADC," alisema.

Majaliwa aliongeza: "Katika hili, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa amempongeza sana Mheshimiwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, wananchi na serikali kwa ujumla katika kuhakikisha Bara la Afrika linabaki kuwa salama."

Kuhusu siasa, Waziri Mkuu alimweleza Katibu Mkuu huyo kuhusu kuwapo Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba, mwaka huu na Uchaguzi Mkuu ujao na kusisitiza haja ya kila mtu kushiriki uchaguzi huo na haki ya kuchaguliwa.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu amepongeza Tanzania kwa jinsi ilivyoshiriki kusaidia Burundi kuwa salama kwa kuendelea kuwapokea wakimbizi katika kipindi chote cha nyuma. Alisema ameridhishwa na hali ya usalama katika ndani ya nchi hiyo na akashauri wakimbizi waanze kurejesha nchini mwao ili waende kuijenga nchi yao na kushiriki kwenye masuala ya maendeleo.

Jana, Waziri Mkuu Majaliwa alitarajiwa kushiriki ufunguzi rasmi wa Mkutano wa 79 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA79) ambako alitarajiwa kujumuika na Wakuu wa Nchi na Serikali kutoka mataifa 193 na pia kutoa salamu za serikali.

Kaulimbiu ya mkutano wa mwaka huu ni "Hakuna kuachwa nyuma yeyote: Kushirikiana pamoja kuendeleza amani, maendeleo endelevu na heshima ya binadamu kwa vizazi vya sasa na vijavyo."

# Sanamu la Mwalimu Nyerere labomolewa, vipande vyaibwa

**Na Benny Kingson,** TABORA

SANAMU la Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere lililoko Kata ya Chemchem, Manispaa ya Tabora limebomolewa na baadhi ya sehemu zake ikiwamo shingo, fimbo pamoja na kiganja kuibwa.

Tukio hilo lilifanywa usiku wa kuamkia Septemba 21, mwaka huu kwenye eneo hilo ambako wahusika hawajajulikana.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Chemchem, Salehe Mbuguma, alisema jana kuwa alipigiwa simu na watu asubuhi akielezwa kutokea kwa tukio hilo na kwamba walikuta sanamu liko chini, huku kichwa kikiwa kimefungwa kwenye kitambaa cheupe, kipande cha nguo ya rangi nyeusi na sarafu ya Sh. 200. Mbuguma alisema sanamu hilo walilikuta likiwa chini na limevunjwa vipande vitatu ambavyo ni kichwa, kiwiliwili cha kuanzia shingoni hadi kiunoni na sehemu ya chini kuanzia kiunoni hadi miguuni na kwamba hawakukuta fimbo ya mfano wa aliyokuwa anashika Mwl. Nyerere.

Diwani wa Mpera, Manispaa ya Tabora, Haruna Msoga, alisema sanamu hilo lina uzito wa kilo 6,000 na lilitolewa jijini Arusha kwenda Tabora mwaka 1988 kwa ajili ya maadhimisho ya sherehe za Chama Cha Mapinduzi (CCM) kitaifa.

Msoga alisema kuwa wakati sanamu hilo linawekwa, eneo hilo lilipandishwa kwa mashine maalum na lilizinduliwa na Mwl. Nyerere.

"Tukio hili si la kiungwana na limetufedhehesha wana Tabora, sanamu hili liliwekwa maalum kwa ajili ya kumbukumbu ya Hayati Mwl. Nyerere, kuenzi harakati zake za kupambania uhuru wa nchi hii na hapa ndipo alipohutubia na kutokwa machozi baada ya kufanyika uamuzi wa busara wa kupigwa kura tatu za kung'oa mkoloni na kujipatia uhuru wetu," alisema.

Aliiomba serikali kufanya uchunguzi wa kina kubaini mwenendo wa tukio zima na kuwakamata wahusika sambamba na kuwachukulia hatua kali za kisheria.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Tabora, Elias Kayandabila, alisema wako katika mchakato wa kuboresha eneo hilo ikiwa ni pamoja na kujenga majengo mapya kwa kuzingatia kuwa "eneo hilo ni nyeti".

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Kamishna Mwandamizi Richard Abwao alisema kuwa wanaendelea na uchunguzi wa tukio hilo kubaini uhalisia wa tukio hilo, kuwatafuta, kuwakamata na kuwafikisha katika vyombo vya kisheria wahusika watakaobainika.

"Tumefika eneo la tukio na kubaini kuwa limeondolewa katika eneo lake la mnara na kuvunjwa vipande vipande, hapa kikubwa tunachunguza ni mazingira gani yamesababisha sanamu hilo linafika chini," alisema Abwao.

Alisema katika uchunguzi wa awali walibaini baadhi ya vipande kutokuwapo na kuwa changamoto ni kuwa eneo hilo halina umeme, pia halikuwa na ulinzi wa aina yoyote.



Mkurugenzi Mtendaji wa Helios Towers Tanzania ambaye ni Mkurugenzi wa Kanda ya Mashariki ya Afrika, Gwakisa Stadi, akishuhudia wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Endevesi wakitumia kompyuta iliyounganishwa na mtandao. Shule hiyo ni ya watoto wa jamii ya wafugaji wa Kimasai iliyoko Oljoro, Arusha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Madaktari bingwa programu ya Samia waokoa maisha mjamzito

**Na Said Hamdani,** LINDI

MADAKTARI bingwa walioko katika programu ya Samia Suluhu Hassan walioweka kambi ya wiki mbili mkoani Lindi, wameokoa maisha ya mjamzito mkazi wa Wilaya ya Ruangwa, mkoani Lindi ambaye mimba ilitunga nje ya kizazi.

Madaktari hao waliosambaa katika wilaya zote tano za mkoa huo, watakuwa wanatoa huduma kwa wananchi wanaokabiliwa na magonjwa mbalimbali.

Akizungumzia tatizo la mwanamke huyo (jina tunalo), daktari bingwa wa magonjwa ya wanawake, uzazi na watoto, Liliani Mnabwiru, alisema mteja wao alifikishwa hosptalini Septamba 17, mwaka huu.

Alisema mteja wao alifikishwa hospitalini huko akiwa na hali mbaya kutokana na kuvuja damu ndani kwa ndani kulikochangiwa na mimba kuwa nje ya nyumba za uzazi.

Bingwa huyo alisema kuwa baada ya kufanyiwa uchunguzi wa kina na kubaini tatizo hilo, walimpa huduma ya dharura ya upasuaji na kuokoa maisha yake.

"Tumempokea akiwa na hali mbaya, tulipomfanyia uchunguzi wa haraka na kubaini mimba aliyobeba iko nje ya nyumba yake ya uzazi," alisema Dk. Mnabwiru.

Alisema kuwa baada ya kubaini tatizo, madaktari walilazimika kumpatia huduma ya dharura kwa mujizi wa mwongozo wa matibabu, ili kuokoa maisha yake na kueleza kuwa hivi sasa hali yake inaendelea kuimarika.

Alisema mimba inapotunga ikiwa nje ya nyumba yake ya uzazi ni hatari kwa usalama wa mama na mtoto kutokana na kukosa mahitaji muhimu katika ukuaji wake, huku akizidi kutoa wito kwa wananchi wenye matatizo kutumia nafasi hiyo kujitokeza kupata matibabu.

Mmoja wa ndugu wa mama huyo, Mauwa Ally, akizungumza na mwandishi wa habari hizi aliyefika hospitalini huko, alishukuru timu ya madaktari hao kuokoa maisha ya dada yake, huku akiomba serikali utaratibu wa kusambaza madaktari hao, wakiwamo mabingwa, mikoani hadi wilayani uwe wa kudumu na si wa muda.

# UDSM yaanza ujenzi wa kampasi mpya ya kilimo

**Na Said Hamdani, LINDI**

CHUO Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kimeanza ujenzi wa kampasi mpya ya kilimo mkoani Lindi.

Imeelezwa kuwa ujenzi huo utatumia miezi 18 kukamilika, ukitajwa kuleta matumaini kwa wananchi kupata fursa za maendeleo na kujikwamua kiuchumi.

Ujenzi wa chuo hicho unaotekelezwa eneo la Ngongo, Kata ya Jamhuri, Manispaa ya Lindi na Kijiji cha Nandagara, wilayani Ruangwa, umefikia asilimia 20.

Naibu Mratibu wa mradi huo, Dk. Liberato Haule, akizungumza na waandishi wa habari waliotembelea eneo la Ngongo, alisema ujenzi umeanza baada ya mkandarasi kukamilisha taratibu za mkataba.

Alisema mradi huo uliopewa unaotekelezwa na mkandarasi kutoka Jamhuri ya Watu wa China, unagharimu Sh. bilioni 13, fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia (WB).

Alisema kuwa ujenzi wa mradi huo ulianza mwezi Julai mwaka huu, ukitarajiwa kukamilika Desemba mwakani, ukihusisha vyumba sita vya madarasa yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 60 kila moja.

Msimamizi wa mradi huo kutoka UDSM, Bahati Thomas, akielezea maendeleo ya ujenzi, alisema unakwenda vizuri, huku akitaja changamoto inayowakabili ni pamoja na upatikanaji saruji kutoka Kampuni ya Dangote ya Mtwara.

"Tunashukuru kazi inakwenda vizuri, changamoto yetu ni upatikanaji wa saruji kutoka Dangote kutokana na kuzidiwa na uhitaji wa wateja," alisema Thomas.

Baadhi ya vibarua wanaoshiriki katika mradi huo, wakiwamo Abdallah Juma, Alphonce Ngajira na Mwajuma Selemani, walishukuru serikali kupeleka fursa hiyo mkoani Lindi' inawasaidia kubadilisha hali zao kiuchumi.

HABARI KITAIFA



Naibu Kadhi Mkuu wa Tanzania, Ali Khamis Ali (wa pili kulia), akimpongeza Shiraz Rashid (wa pili kushoto), aliyejenga Msikiti wa Masjid Imam Ali Bin Abu Talib eneo la Magomeni, Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa msikiti huo jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Migongano baina ya binadamu na wanyamapori yaendelea kupungua

**Na Jenifer Gilla**

MIGONGANO kati ya binadamu na wanyamapori imepungua katika Kijiji cha Kitanda, wilayani Namtumbo kutoka kesi 46 zilizoripotiwa mwaka 2023 hadi 15 mwaka huu.

Sababu za kupungua kwa migongano hiyo ni pamoja na elimu juu ya njia salama za kujikinga na wanyamapori pamoja na vifaa vya kujikinga vinayotolewa na serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo.

Akizungumza na waandishi wa habari wanachama wa Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET), Mwenyekiti kijiji hicho, Joseph Ngonyani, alisema wiki iliyopita kuwa serikali imekuwa inashirikiana na wadau kudhibiti tembo kuvamia mashamba yao na kufanya uharibifu.

Alisema miaka ya nyuma tembo walikuwa wanaingia katika mashamba ya wakulima na kula mazao kwa kiasi kikubwa kwa kuwa hawakuwa na njia nzuri ya kujikinga, zaidi ya kuwafukuza na baadaye walirudi tena.

Alisema kuwa mwaka jana, serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ) waliwapa elimu namna ya kutengeneza dawa yenye harufu kali na kuiweka pembezoni mwa mashamba yao kuzuia tembo kuingia na kufanya uharibifu.

Alisema walianza kuzungushia dawa hiyo kwenye mashamba yaliyo jirani na hifadhi kwa kuwa ndiko kulikokuwa na matukio mengi ya uharibifu ambapo sasa yamepungua kwa kiasi kikubwa.

Alisema tangu walipoweka dawa hiyo, matukio ya tembo kuvamia mashamba yamepungua kutoka 46 aliyopokea mwaka 2023 hadi 15 mwaka huu, maeneo yanayovamiwa ni yale ambayo hayajawekewa 'uzio' wa dawa hiyo.

"Tunawashukuru GIZ yale mashamba yaliyozungushiwa hiyo dawa hakuna hata moja lililovamiwa na tembo, wenye yale mashamba mwaka huu wanapata mavuno mazuri kulinganisha na mwaka jana," alisema.

Ofisa Mtendaji wa kijiji hicho, Edson Ndungule, alisema shirika hilo pia linawapatia mafunzo askari wa uhifadhi wa kijiji ili kuwaongezea mbinu za kukabiliana na wanyama hao katika kijiji hicho.

Aliomba shirika hilo kuongeza askari wenye mafunzo na kuwapa posho pamoja na vitendea kazi ili kuwaongezea morali ya utendaji kazi kwa kuwa hivi sasa wanajitolea na hawalipwi chochote.

Ofisa Kilimo wa Kata ya Kitanda, Wilson Ngerangera, alisema wanaendelea kushirikiana na GIZ kuweka uzio wa dawa yenye harufu kali kwenye mashamba ambayo hayajafikiwa na teknolojia hiyo.

Alisema wanaendelea kutoa elimu kwa wanakijiji na kuwashawishi wale wanaolima na kulisha mifugo ndani au karibu ya hifadhi kinyume cha sheria wahame kwa kuwa ni moja ya vichocheo vya migogoro.

Mmoja wa wakulima katika kijiji hicho, Afuna Nyoni, alishukuru GIZ kwa kuwapa mbinu salama za kukabiliana na tembo katika mashamba yao kwa kuwa imeepusha hasara aliyokuwa anapata awali.

Alisema kuwa mwaka jana alilima ekari mbili za mahindi, lakini tembo walivamia na kuharibu ekari moja na nusu, hali iliyomwathiri kiuchumi, lakini mwaka huu hakukuwa na madhara yoyote katika shamba hilo kwa kuwa aliweka uzio wa dawa ya kudhibiti wanyama hao.

Alishauri serikali iwahamishe wafugaji wanaolisha mifugo ndani ya hifadhi kwa kuwa wanasababisha wanyamapori kukimbilia katika mashamba yao wakiikimbia mifugo hiyo.

Mratibu Mshauri wa GIZ Wilaya ya Namtumbo, Chrian Zimbaiya, alisema Kitanda ni moja ya vijiji vinane wanakotekeleza mradi wa miaka mitatu ulioanza mwaka 2022, ukilenga kumaliza migongano kati ya binadamu na wanyamapori kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii.

Alisema kupitia mradi huo, wanajengea uwezo Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo namna ya kukabiliana na wanyama waharibifu.

Mratibu huo alisema wanaipa ruzuku halmashauri hiyo kwa ajili kuwasaidia watendaji wake kuweka mafuta kwenye magari na kuwapa posho askari wa wanyamapori wa vijiji ili kuwarahisishia utendaji kazi wanapokwenda kutekeleza majukumu ya uhifadhi.

Alisema kuwa pia wanawapa vitendea kazi kwa ajili ya utekelezaji shughuli hizo, zikiwamo pikipiki, kompyuta na vile vinavyohitajika kufukuza tembo kama vile dawa zenye harufu kali.

# Watendaji maabara uchunguzi wa sayansi jinai wapewa angalizo

**Na Maulid Mmbaga**

NAIBU Kamishna wa Polisi, Mwamini Rwantale, amewataka watendaji wa Jeshi la Polisi katika maabara za uchunguzi wa sayansi jinai kuzingatia weledi na maadili wakati wa utekelezaji shughuli zao ili kuepuka majibu yao kutiliwa shaka.

Kamishna Mwamini ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Sayansi Asilia ndani ya jeshi hilo, alisema mwishoni mwa wiki kuwa majibu na vielelezo vya wataalamu hao kuhusu makosa ya jinai vinategemewa kutenda haki kwa jamii na vyombo vya uamuzi, ikiwamo mahakama katika kufanya uamuzi wa kisheria.

Akizungumza mkoani Dar es Salaam katika maadhimisho ya Siku ya Uchunguzi wa Kisayansi wa Makosa ya Jinai (Forensic Day) ambayo kwa Tanzania ni mara ya kwanza kuadhimishwa, alisema itakuwa aibu majibu ya wataalamu kutoka maabara ya uchunguzi wa sayansi jinai yakitiliwa shaka na kufanyiwa uchunguzi tena ili kujiridhisha.

Alisema ni muhimu kwa wataalamu wa tasnia hiyo kuzingatia maadili kwa kuwa Jeshi la Polisi liko katika awamu ya pili ya maboresho ya utendaji kazi na utekelezaji mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai iliyoundwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

"Sayansi imekuwa na mchango mkubwa kwenye maisha ya binadamu katika kusaidia haki kutendeka, kwani kupitia uchunguzi wa sayansi jinai tumeshuhudia wahalifu wakibainika kirahisi, na kuunganishwa na tuhuma zinazowakabili pasipo shaka, huku wasio na hatia wakiachiwa huru.

"Mnaweza kuona ni kwa kiasi gani pale dunia itakapokuwapo pasipo ukweli, tutashuhudia wahalifu wakiachiwa huru, na wasio na hatia wakifungwa gerezani.

"Hivyo, tunaadhimisha siku hii muhimu kama sehemu ya mapinduzi ya sayansi kwenye mchakato mzima wa utoaji haki," alisema Kamishna Mwamini.

Alieleza kuwa siku hiyo inaashiria kuwatambua mashujaa na wagunduzi wa uchunguzi wa kisayansi waliofanya kazi kubwa katika kuhakikisha sayansi inakwenda kutoa mchango wake kwenye mchakato mzima wa utoaji haki.

Alisisitiza kuwa bila jitihada hizo, upatikanaji haki duniani ungeendelea kubaki kuwa ndoto. Pia alisema linapokuja suala la utafutaji haki, kila kitu kwenye eneo la tukio kina umuhimu mbele ya sayansi, akisema unywele mmoja, tone la damu, mwandiko kwenye karatasi na mambo mengine yanayohusiana, vyote ni muhimu katika kubaini ukweli.

Naibu Kamishna huyo alisema tasnia hiyo ni muhimu katika dunia ya leo hasa katika kubainisha ukweli na kusaidia haki kutendeka katika jamii.

"Sisi kama wadau wa uchunguzi wa sayansi ndani ya Jeshi la Polisi tunaamini katika kusherehekea siku hii inaonesha umuhimu wetu katika jamii, na imekuja kipindi mwafaka cha kuboresha utendaji wetu, ikiwamo kubadilika kifikra, kutenda kwa weledi na kuacha utendaji wa mazoea," alisema Kamishna Mwamini.

Mwakilishi kutoka Maabara ya Sayansi Jinai Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Fidelis Segumba, alisema katika utendaji wa shughuli zao, wanashirikiana na Jeshi la Polisi, akisisitiza kuwa ni muhimu kwa wataalamu wa eneo hilo kuzingatia weledi tangu wanapoanza kuchukua sampuli, kuzitenganisha vizuri hadi wanakozifikisha ili kuondoa mkanganyiko.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Watendaji viwanja vya CCM wasimkwamishe Rais Samia

**TANZANIA** ni moja kati ya timu ambazo zitakuwa mwenyeji wa Fainali za Mataifa Afrika kwa Wachezaji wanaocheza Ligi Ndani (CHAN), Februari mwakani, lakini pia itakuwa mwenyeji wa Fainali za Mataifa ya Afrika, (AFCON) 2027.

Nchi zingine zitakazoshirikiana na Tanzania kuandaa fainali hizo mbili ni Kenya na Uganda.

Moja ya vitu ambavyo vinahitajika na vimeshaanza kufanyiwa kazi ni miundombibu ya viwanja na vitu vingine kama malazi, usafiri na mengine yanayofanana na hayo.

Tayari kuna ujenzi wa viwanja vipya, pamoja na kuvikarabati vya zamani ambavyo vitaonekana vinafaa kwa ajili ya michuano hiyo, lakini pia kutumika kwa mazoezi.

Haya yote yanafanyika kutokana na mapenzi ya michezo aliyonayo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, ambayo hayafichiki.

Rais amejipambanua kuwa mpenzi wa michezo mbalimbali na hata kukubaliwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), Tanzania kuwa miongoni mwa nchi za Afrika Mashariki kuandaa fainali hizo, ni kutokana na juhudi zake.

Tukumbuke wakati wa maombi ya uenyeji kulikuwa na mataifa mengine makubwa kimpira Afrika yaliyoomba, lakini ile Rais Samia kuonekana yupo mstari wa mbele kutaka Tanzania kuwa mwenyeji, ilitosha kabisa kuonesha kuwa AFCON itakuwa salama zaidi itakapopigwa nchini, pamoja na washirika wake nchi za Kenya na Uganda.

Ikumbukwe mbali na kuwa rais, Dk. Samia pia ndiye Mwenyekiti wa chama tawala, CCM ambacho kinamiliki viwanja vingi zaidi nchini.

Hivyo, wakati rais akionekana kuwa na nia ya dhati ya kuendeleza michezo si uwanjani tu hata kwenye miundombinu, lakini baadhi ya watendaji wake hasa kwenye chama tunasikitika tukiona wanamwangusha.

Hii ni kutokana na ukweli kwamba, viwanja vinavyomilikiwa na CCM ndiyo mara kwa mara vinafungiwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), kwa kutokidhi vigezo vya kutumika kwenye Ligi Kuu na kukumbushwa kuvifanyia maboresho na baadaye vinafunguliwa kabla ya kufungiwa tena.

Haya yamekuwa ni maisha ya kawaida kwenye viwanja hivi ambavyo mwisho wake haujulikani, ni lini vinaweza kuwa miongoni mwa viwanja vinavyotunzwa vema na kuweza kutumika kwa msimu mzima bila kufungiwa.

Na ikifuatiliwa utakuta mara nyingi vinaharibika kutokana na kuruhusu matamasha kufanyika eneo ambalo mpira unachezwa.

Hatukatai wala kuwapanga kwa matumizi kama hayo, lakini wasimamizi hao wangeweza kufanya hivyo bila kuathiri eneo la kuchezewa.

Viwanja vingi vya CCM vina eneo la kukimbilia, hivyo matamasha yangeweza kufanyika hapo bila mashabiki kugusa nyasi viwanjani.


Tumesikia kuwa mbali na kujengwa viwanja vipya, lakini vingine vitakarabatiwa kwa ajili ya michuano hiyo, pia vipo vitakavyokarabatiwa ili timu zitakazokuja zifanyie mazoezi wakati zipo hapa nchini.

Tunaona huu ndiyo wakati sasa wa kuvifanyia maboresho makubwa viwanja vyote ambavyo asilimia zaidi ya 90 ni vya nyasi asili, na watendaji kumuunga mkono Rais Samia kwa kuvitunza na kutoacha viharibike mara kwa mara kwa matamasha.

Lakini pia, iwapo vitapatikana viwanja vipya, vingine vikarabatiwa, na vyote vinavyomilikiwa na CCM ambavyo ni vingi zaidi nchini vitafanyiwa matengenezo makubwa, hivyo uzingatiaji utunzaji, nadhani Tanzania itakuwa moja ya nchi yenye viwanja vingi bora zaidi Afrika.

Huu ni wakati sasa kwa watendaji wote wa chama tawala na nje ya chama hicho, wote kwa pamoja kushirikiana katika utunzaji wa viwanja hivyo na si eneo la kuchezea tu, bali hata miundombinu ya viwanja hivyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# CAF itoe adhabu ya kuziondoa mashindanoni timu zenye fujo

**IMEANZA** kuwa ni kawaida sasa kwa timu kufanyiana fujo kwenye michezo ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Kwa miaka ya hivi karibuni, mchezo ule wa timu za Afrika Kaskazini kuzifanyia fujo timu zinazokwenda kucheza michezo ya kimataifa kwao imeanza kurejea tena.

Miaka ya 1960 hadi 1970, mpaka 1990 ilikuwapo, lakini baada ya kupewa adhabu ikiwamo mashabiki wao kufungiwa kutoingia viwanjani, na wakati mwingine timu zao kutoruhusiwa kucheza nchini kwao, na hata kutolewa kwenye michuano ilizaa matunda na klabu hizo kuanza kuwa na nidhamu.

Cha kushangaza kwa miaka ya karibuni umeanza kuzuka mchezo huu, ambayo si wa kiungwana hata kidogo katika kile ambacho FIFA wanakiita 'fair play'.

Mfano tuliona wachezaji wa Simba na baadhi ya viongozi wao walivyofanyiwa katika mchezo wa Kombe la Shirikisho Afrika, kwenye Uwanja wa Juni 11 jijini Tripoli, ilipocheza dhidi ya Al Ahli Tripoli nchini Libya.

Kulizuka vurugu kubwa, ambapo kwa mujibu wa Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema wachezaji wao walianza kufanyiwa fujo na mashabiki, kabla ya mchezo na hata mchezo ulivyokuwa unaendelea hasa kule pembeni wakati wa kwenda kurusha mpira au kupiga kona, walikuwa wakirusha makopo na chupa za plastiki.

Kasheshe ilikuwa kubwa pale mechi ilipomalizika na mashabiki kushindwa kupata kile walichotarajia kutoka kwa timu yao, ilipotoka suluhu.

Ilibidi wanausalama kuwakimbiza wachezaji wa Simba vyumbani, lakini katika namna ya kushangaza, kule jukwaani nako baadhi ya viongozi walifanyiwa fujo, huku ikidaiwa mwanausalama mmoja akimpiga Aishi Manula aliyekuwa amekaa jukwaani.

Hata hivyo, tayari Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), Patrice Motsepe, ameagiza kufanyika uchunguzi dhidi ya vurugu hizo.

Klabu ya Simba nayo ikaamua kutuma mlalamiko CAF dhidi ya Al Ahli Tripoli juu ya kurushiwa chupa za maji za plastiki, lugha mbaya, matusi, maneno ya kibaguzi na kushambuliwa kwa wachezaji na baadhi ya viongozi wa timu hiyo.

Wakati hayo yakiendelea kulizuka vurumai kubwa juzi katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika kati ya MC Alger ya Algeria na US Monastir ya Tunisia.

Kwenye mchezo wa marudiano uliochezwa nchini Algeria, MC Alger ilishinda mabao 2-0 na kutinga makundi kwa jumla ya mabao 2-1, kwani katika mchezo wa kwanza ilipoteza nchini Tunisia kwa bao 1-0.

Kulizuka tafrani kubwa kuanzia uwanjani, mpaka kwenye vyumba vya kuvalia. Mimi naona umefika wakati kwa CAF kuziondoa mashindanoni timu zote ambazo mashabiki wake wanafanya fujo, au viongozi kuwafanyia vurugu wageni wao.

Hii nadhani inaweza kuwatia woga kuliko kuzipiga faini kwani inaonekana wala hazihofii chochote na wanaweza kufanya lolote kwa sababu faini ya fedha kwao si tatizo kulipa.

Ikumbukwe timu zinazofanya hivi nyingi ni za Afrika Kaskazini, ambazo ziko vizuri sana kiuchumi, hivyo zinajua zitafanya fujo kwa maslahi ya timu zao na zitalipa faini.

Hebu angalia, baada ya kuona kuwa imewafanyia fujo Simba, yenyewe Al Ahli Tripoli ikajihami kwa kukodisha mabaunsa ilipokuja nchini kwenye mechi ya marudiano.

Imefika wakati sasa CAF kuchukua hatua ya kuzipa adhabu kali klabu za aina hii kwani kuziacha ni kuonekana kama inaziogopa. Na tabia hii ikiendelea ipo siku yatatokea maafa makubwa uwanjani. CAF isisubiri majeruhi au vifo ili ichukue hatua.

HABARI KITAIFA

## Mahakama Kuu yajipanga kesi mabadiliko ya tabianchi

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania imejipanga kushughulikia mashauri yatakayotokana na uharibifu wa mazingira, yakiwamo yanayohusiana na mabadiliko ya tabianchi.

Sambamba na hilo, Mahakama Kuu imeanza kujipanga kutumia nishati mbadala kwenye mahakama zake ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira.

Hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki mjini hapa na Jaji wa Mahakama Mkuu Tanzania Kitengo cha Uboreshaji Mahakama, Dk. Angelo Rumisha.

Ni wakati akitoa taarifa ya utekelezaji Mkakati wa Miradi ya Maboresho katika Utoaji Huduma Mahakamani kwa waandishi habari wa Mkoa wa Morogoro.

Jaji Dk. Rumisha alisema kuwa kutokana na mabadiliko ya tabianchi, tayari kumeanza kuonekana viashiria vya kuwapo mashauri hayo, hivyo nao wameshajipanga kwa ajili ya kuyasikiliza.

"Ninatolea mfano, mimi mwaka 2000 nilikuwa ninaishi hapa Morogoro, sikuwahi kuona ule Mlima Uluguru ukiwa ulivyo hivi sasa.

"Hivyo, tunaona lazima tujiandae kama mahakama, muda si mrefu tutapata mashauri yanayohusiana na mabadiliko ya hali ya hewa na mabadiliko ya tabianchi," alisema Jaji Dk. Rumisha.

Alisema mabadiliko ya tabianchi yanaweza kusababisha vitu vingi ikiwamo kuvunjwa kwa nyumba au kubomolewa kwa miundombinu mbalimbali, hivyo ni lazima kama mahakama waanze kujindaa kupata mashauri hayo.

Kuhusu matumizi ya nishati mbadala kuanza katika mahakama, Jaji Dk. Rumisha alisema kuwa hivi sasa matumizi ya nishati nchini yamekuwa yanaongezeka kila mwaka, hata wao wamekuwa na matumizi madogo, hivyo kuanzia sasa majengo yao watahakikisha yanawekwa nishati mbadala.

Kuhusu uboreshaji huduma za mahakama, Jaji Dk. Rumisha alisema mfumo wa kieretroniki umepunguza kwa kiasi kikubwa mrundikano wa majalada ya kesi pamoja na malalamiko kutoka kwa wananchi.

"Hivi sasa hakuna tena majalada yanayotembea kwenye mahakama zetu zote kwani tunatumia mfumo wa kielektroniki ambapo kila kitu kinachofanyika kinaonekana na hii imetusaidia kuondoa malalamiko kabisa," alisema Jaji Dk. Rumisha.

Merina Mhamaka, mkazi wa Kata ya Mji Mkuu, mjini hapa, alipongeza huduma za mahakama, akieleza kuwa hivi sasa zimeboreshwa katika Kituo Jumuishi cha Utoaji Haki kutokana na kila mwananchi kupangiwa muda wa kusikiliza kesi yake tofauti na awali wananchi walikuwa wakifika kuanzia asubuhi na kushinda mpaka jioni kusubiri kesi zao.

"Sasa hivi kama una kesi pale Mahakama Kuu, unaambiwa kabisa kesi yako itakuja kusikilizwa siku fulani, muda fulani, mfano saa saba mchana.

"Hii ni tofauti na awali, ulikuwa unakwenda mahakamani kuanzia asubuhi kesi inasikilizwa jioni, mnajikuta mnapoteza muda bure," alisema Merina.

Mkazi wa Kata Kihonda mjini hapa, Christer Kumburu, akizungumzia huduma za mahakama, alisema mahakama kwa sasa zinatoa huduma nzuri kulingana na changamoto ambazo wananchi wanakutana nazo.



Mamalishe mkazi wa Kijiji cha Makamaka, wilayani Chemba, Amina Athumani, akipika uji kwa ajili ya wateja wake, ambapo kikombe kimoja kiliuzwa kwa bei ya Sh. 500. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Kikwete kuongoza harambee ya matibabu ya moyo watoto 1,500

**Na Joseph Mwendapole**

RAIS mstaafu wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete anatarajiwa kuongoza harambee ya kuchangia matibabu ya watoto 1,500 wanaougua magonjwa mbalimbali ya moyo ili wapate matibabu katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI).

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam na Naibu Spika wa Bunge, Musa Zungu, wakati akizungumzia harambee hiyo inayotarajiwa kufanyika tarehe 2 Novemba, mwaka huu, jijini Dar es Salaam.

Alisema takwimu za Wizara ya Afya zinaonesha kuwa kati ya watoto 100 wanaozaliwa, wawili wanakuwa na matatizo ya moyo na kwamba hadi sasa watoto 1,500 wameandikishwa kupata matibabu hayo, lakini wazazi wao hawana uwezo kifedha.

Naibu Spika Zungu ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Heart Team Africa Foundation, alisema watoto hao wasipopata matibabu hayo kwa wakati, wanaweza kupoteza maisha, hivyo amewaomba Watanzania kujitokeza wakati wa harambee hiyo kuchangia fedha kwa ajili ya gharama za matibabu.

"Ninawaomba Watanzania tuungane kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan katika juhudi zake za kuimarisha huduma za mama na mtoto.

"Serikali yake imekuwa inachangia asilimia 70 ya gharama ya matibabu kwa watoto wanaozaliwa na matatizo ya moyo, hivyo ni wakati mwafaka wa kumuunga mkono Rais wetu," alisema.

Zungu alisema watoto wengi wenye matatizo hayo wanatoka familia zisizo na uwezo kifedha, hivyo aliomba taasisi na mashirika mbalimbali kujitokeza kusaidia juhudi za serikali kugharamia matibabu ya watoto hao ili wakatibiwe JKCI. Alisema JKCI kwa kushirikiana na Taasisi ya Heart Team Africa Foundation wameandaa harambee hiyo kwa ajili ya kukusanya asilimia 30 ya matibabu ya watoto hao ambayo ni sawa na Sh. milioni nne kwa kila mtoto atakayetibiwa.

"Ninawaomba Watanzania wote, wafanyabiashara, taasisi binafsi na za umma, vilabu vya michezo, wasanii, mabalozi wa nchi mbalimbali na vyombo vya habari tuunge mkono juhudi hizi za serikali katika harambee hii ya kuokoa maisha ya watoto wetu," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa JKCI, Dk. Peter Kisenge alimpongeza Rais Samia kwa serikali kuendelea kuwekeza kwa kiasi kikubwa katika sekta ya afya kwa kununua vifaa vya kisasa vya matibabu kwa hospitali zote kubwa nchini pamoja na kusomesha wataalamu bobezi. Dk. Kisenge alisema uboreshaji huduma za afya nchini umewavutia wagonjwa wa nchi mbalimbali ambao wamekuwa wakienda JKCI kupata matibabu ya kibingwa.

"Ninamshukuru na kumpongeza Rais Samia kwa maono makubwa aliyonayo kwa sekta ya afya kwani ameendelea kuwekeza kwenye sekta ya afya ambapo mabadiliko makubwa sana yametokea kiasi kwamba vifaa vya kisasa ambavyo tulilazimika kuvifuata nje ya nchi, sasa vinapatikana katika hospitali zetu nchini," alipongeza.

KABWELA — FADHILI MOHAMED



# Wafugaji waanzisha kijiji cha utalii

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

WAFUGAJI wa kabila la Kimasai wametumia fursa ya kuwapo Hifadhi ya Taifa Mikumi (MINAPA) wilayani Kilosa, mkoani Morogoro kuanzisha Kijiji cha Utalii wa Kitamaduni wa kabila hilo walichokipa jina la "Mikumi Masai Boma".

Utalii huo wa kitamaduni unapatikana katika Kijiji cha Kikwalaza, Mikumi ambako watalii wanapata fursa ya kujifunza mambo mbalimbali ya kabila la Wamasai.

Akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki, Mratibu wa Mikumi Masai Boma, Nuhu Mereni, alisema wameamua kuanzisha utalii huo ili kuwavutia zaidi wageni wanaotembelea Hifadhi ya Taifa ya Mikumi kujua utamaduni wa kabila hilo, ukijumuisha vyakula wanavyotumia.

Alisema watalii hao wanapofika katika Kijiji cha Utalii cha Mikumi Masai Boma, kwanza wanavalishwa mavazi ya kimasai, watapekechewa moto na kupewa historia ya kabila hilo pamoja na michezo mingine, ikiwamo ngoma.

Mratibu huyo wa Mikumi Masai Boma alisema kuwa, pamoja na mambo mengine, watalii hao watapata fursa ya kufundishwa kuchunga ng'ombe na kuoneshwa makazi ya kijadi ya kabila hilo.

"Tunashukuru kuwapo hifadhi hii ya Mikumi na sisi kama wafugaji wa kabila la Kimasai wa wilayani Kilosa, tukatumia fursa hiyo kuonesha utamaduni wetu ambao wageni wanaotembelea hifadhini, wamekuwa wanapendezwa nao na kuingiza mapato - fedha," alisema Nuhu.

Mwanzilishi wa Utalii wa Utamaduni nje ya Hifadhi ya Taifa Mikumi, Makene Ngoromo, alisema kuwa wameanzisha utalii mpya wa kitamaduni wa kabila la Wavidunda wanaoishi pembezoni mwa Hifadhi ya Taifa Mikumi na Udzungwa.

Alisema kupitia utalii huo wa Wavidunda, waliainisha vivutio mbalimbali, zikiwamo aina tano ya maporomoko ya maji ambayo yanapatikana katika Milima ya Wavidunda iliyoko katika Milima ya Tao la Mashariki.

Alisema kuwa katika milima hiyo pia wanaishi kabila hilo la Wavidunda ambao maisha yao yamekuwa kivutio pamoja na mazao yao ya kilimo katika milima hiyo ambayo ni kivutio kikubwa kwa watalii wengi.

Mkuu wa Hifadhi ya Taifa Mikumi, Augustine Masesa, alisema hifadhi hiyo ni moja ya alama za uhifadhi zilizorithiwa toka kwa wazee, ikiwamo bayonuai na wanyamapori, hivyo imeona pia umuhimu wa kutoa fursa kwa utalii wa utamaduni wa makabila mbalimbali yanayozunguka eneo hili ili kuongeza kipato.



Naibu Waziri wa Viwanda, Exaud Kigahe, akitia saini kitabu cha wageni alipotembelea banda la Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) katika Tamasha la Maonesho ya Kariakoo (Kariakoo Festival) yaliyofanyika Viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Serikali kuunga mkono ubunifu wa YST

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI itaunga mkono programu ya Taasisi ya Wanasayansi Chipukizi (YST) ya kuibua wanafunzi wenye vipaji vya kufanya ubunifu wa kuleta suluhisho katika jamii.

Mwishoni mwa wiki, jijini Dar es Salaam, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, alitoa kauli hiyo wakati akitoa tuzo kwa wanafunzi waliofanya vizuri kupitia ugunduzi wa utafiti wa kisayansi, zilizoandaliwa na YST.

Alisema kwa hivi sasa serikali imeweka nguvu kubwa kuwekeza katika sayansi na teknolojia kutokana na umuhimu wake katika uchumi wa viwanda.

"Ninachukua nafasi hii kuwapongeza washiriki wote ambao wamekuwa wanashirikiana na Taasisi ya YST tangu mwaka 2011 na kuwadhamini wanafunzi kufanya ubunifu mbalimbali na hatimaye kupata ushindi," alisema Prof. Mkumbo.

"Kwa sasa Tanzania inaandaa Dira ya Taifa ya kwenda mpaka mwaka 2050. Moja ya maeneo yanayotiliwa mkazo wa dira hiyo kama kichocheo cha maendeleo ya uchumi ni masuala ya sayansi na teknolojia," alisema.

Alipongeza YST kwa kujitoa kuibua vipaji kwa wanafunzi hao, ikiwamo kutoa ufadhili wa masomo ya chuo kikuu kwa wanafunzi wanaofanya vizuri zaidi kupitia wadhamini wake Karimjee Foundation.

Mwenyekiti wa Bodi ya YST, Prof. Yunus Mgaya, alisema taasisi hiyo imetoa fursa kwa vijana kuonesha kazi zao kama jukwaa la kushindana na kuonesha vipaji vyao kama sehemu ya kuhamasisha sayansi na ubunifu kwa wanafunzi kwenye shule za sekondari nchini. Alisema mashindano hayo ni ya 14 tangu yaanzishwe na yamesaidia kuwajengea wanafunzi uwezo katika kupenda sayansi ili kupata wataalamu ambao watakuwa wahandisi, madaktari na wataalamu wa sekta mbalimbali.

Mwakilishi kutoka Taasisi ya Karimjee Foundation ambao ni miongoni mwa wadhamini wakuu wa ugunduzi hizo, Cobus Van Zyl alisema wataendelea kutoa ufadhili wa masomo ya elimu ya juu kwa wanafunzi wanaofanya vizuri.

"Wanafunzi wengi waliopata ufadhili wetu, hivi sasa wamekuwa madaktari, wahandisi na wanasayansi wanaofanya mabadiliko makubwa nchini.

"YST wamekuwa wanafanya tukio la kipekee kwa kutoa jukwaa kwa vijana kutoka mikoa mbalimbali Tanzania kuonesha ubunifu, ugunduzi, utafiti pamoja na taranta zao za kisayansi. Tunawapongeza kwa hilo," alisema Van Zyl.

# RC aagiza watendaji kutoa elimu ya Uchaguzi S/Mitaa

**Mussa Mwangoka, MPANDA**

MKUU wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko amewaagiza watendaji wa serikali ngazi za halmashauri, kata, vijiji, vitongoji na mitaa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu utofauti wa Daftari la Kudumu la Wapigakura na lile la makazi litakalotumika katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Amesema kufanya hivyo kutawasaidia wananchi hao kushiriki katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na kuwachagua viongozi wanaotaka ambao watawaongoza kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Alisema hayo jana wakati wa kikao kazi kilicholenga kufanya tathmini ya utendaji kazi katika mwaka wa fedha uliopita kilichofanyika kwenye Ukumbi wa Manispaa, mjini Mpanda, mkoani hapa.

Alisema wapo Watanzania wanashindwa kutofautisha ni daftari lipi linatumika kwenye uchaguzi huo, hivyo ni wajibu wa watendaji kutoa elimu ili wasipate mkanganyiko na kushindwa kushiriki zoezi la upigaji kura wa kuchagua viongozi wao.

Aliwaomba wananchi kujiandikisha kwa wingi kwenye daftari hilo litakalowawezesha kupata sifa ya kupiga kura kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Mkuu wa Mkoa alisema kadi ya mpigakura itatumika tu kwenye Uchaguzi Mkuu mwakani, lakini Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wananchi wanatakiwa wakajiandikishe kwenye daftari la mkazi kuanzia Oktoba 11 hadi Oktoba 20, 2024.

"Ili uwe na sifa ya kumchagua kiongozi umtakaye kwenye Uchaguzi huu wa Serikali za Mitaa, ni lazima ukajiandikishe kwa muda wa siku 10 zilizotolewa kupitia tangazo lililotangazwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa," alisema.

Ofisa wa Serikali za Mitaa Mkoa wa Katavi, Gwamaka Owden, alisema mchakato wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaendelea vizuri kwa kufuata ratiba iliyotolewa na serikali kupitia Ofisi ya Rais - TAMISEMI.

**"Ili uwe na sifa ya kumchagua kiongozi umtakaye kwenye Uchaguzi huu wa Serikali za Mitaa, ni lazima ukajiandikishe kwa muda wa siku 10 zilizotolewa kupitia tangazo lililotangazwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa," alisema.**



## Wanawake wapewa mafunzo utambuzi wa fursa

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MRADI wa sauti ya haki, umeanza kuwanoa wanawake ili waweze kutambua fursa mtawalia, kuzichakata na kushiriki mchakato wote wa uzalishaji na matumizi sahihi ya rasilimali, kwa ajili ya maendeleo pamoja na kujiimarisha na kuongeza kipato halali.

Mradi huo wa miezi sita, unaotekelezwa na Shirika la KWIECO, kwa ufadhili wa Women Fund Tanzania Trust (WFT), unalenga kuendeleza majukwaa ya wanawake kwa ajili ya haki za uongozi kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji utakaofanyika Novemba 27, mwaka huu.

Akizungumza mwishoni mwa wiki na makundi hayo kutoka Kata ya Pasua, Ofisa Ufuatiliaji, Tathmini na Taarifa wa Shirika hilo, Peter Mashingia, aliwataka wanawake na vijana wenye nia ya kugombea katika uchaguzi huo, kutambua wajibu huo.

"Unapotaka kugombea hizi nafasi, hebu waza utatengenezaje mifumo ya kuhakikisha kwamba kuna upatikanaji wa fursa mtawalia, ili vijana na wanawake waweze kunufaika na hizo fursa," alisema.

Kabla ya kikao hicho cha wadau, Mratibu wa mradi huo, Veronica Ollomi, alisema pamoja na uchaguzi, mradi huo utashughulikia uimarishaji haki za kifeminia na haki za kijamii.

Kwa mujibu wa Ollomi, kata zilizolengwa kujengewa uwezo ni Pasua na Ngangamfumuni (Manispaa ya Moshi), na Mabogini, Mwika Kusini, Mwika Kaskazini na Kirua Vunjo (Halmashauri ya Wilaya ya Moshi).

"Tunaelekea katika mchakato wa uchaguzi, tumeona tuje tujengeane uwezo. Hatuangalii chama, tunawajengea uwezo watu wote wale ambao wenye nia ya kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

Zaidi aliongea: "Na hata tulivyotoa taarifa kwa Mtendaji wa Kata na waliohusika kuwaita tuliwaambia kwamba sifa ya kwanza au kigezo cha kwanza, awe ana nia ya kutamani kushiriki kwenye mchakato wa kuogombea nafasi za uongozi katika uchaguzi wa serikali za mitaa".

# Ulevi, ubakaji, ulawiti bado tatizo Kilimanjaro

**Na Mary Mosha**, MOSHI

KAIMU Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Jenerali Mstaafu, James Kaji amesema vitendo vya ulevi uliokithiri, ubakaji na ulawiti vimeshika kasi mkoani Kilimanjaro.

Hivyo, amewataka maofisa ustawi wa jamii kujadili namna ya kutokomeza vitendo hivyo ili kusaidia ukuaji na ustawi wa nguvu kazi ya taifa.

Alisema hayo juzi katika mkutano wa maofisa ustawi wa jamii, uliofanyika katika Shule ya Polisi Tanzania (TPS), kuwataka maofsa ustawi kujadili na kuona namna ya kukomboa mkoa huu kwa matatizo hayo.

"Tunaomba mlijadili kwa kina, maana hili ni tatizo jipya ambalo linadidimiza nguvu kazi ya taifa. Ni tatizo linalohitaji malezi, na viongozi wa dini. Lakini lipo lingine linalokuja kwa kasi ni vitendo ya ubakaji na ulawiti, limekuwa ni tatizo kubwa na wenzetu wa Jeshi la Polisi na maofsa ustawi wamekuwa kwenye mazingira magumu kutokana na familia kuwatunza watuhumiwa na hawatoi ushirikiano," alisema Kaji. Alisema wiki iliyopita walipata kesi katika Wilaya ya Moshi ya watoto watatu kulawitiwa ila wazazi wakagoma kutoa ushirikiano hali iliyopelekea kuwakamata wazazi kwa uchunguzi zaidi.

Aidha baadhi ya viongozi wa dini, akiwamo Shehe wa Mkoa wa Kilimanjaro, Shaban Mlekwa, aliwataka vijana kujikita katika kufuata maadili ya kiafrika ikiwa ni pamoja na kuoa na kuolewa.

Baadhi ya wananchi wa Machame Uroki, akiwamo Anael Nkya (83) alizungumzia suala la ulevi na kusema kuwa hilo limekuwa tatizo kubwa na kuiomba serikali kufanya msako kwenye maduka yote hasa vijijini, kuondoa biashara hiyo na kuruhusiwa kwenye maeneo yenye leseni ya biashara ya vileo.



Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Tanga, Rajabu Abdallah, akizungumza katika dua maalum iliyoandaliwa na chama hicho mkoani Tanga katika Msikiti wa Ijumaa ya kumwombea Ali Kibao aliyekuwa kada wa CHADEMA aliyefariki dunia hivi karibuni baada ya kutekwa na watu wasiojulikana kisha kuuawa kikatili na kutupwa eneo la Ununio, Dar es Salaam. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Serikali kuanzisha idara ya ustawi wa jamii inayojitegemea

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SERIKALI imesema ipo katika hatua za mwisho kuanzisha idara ya ustawi wa jamii inayojitegemea chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Makundi Maalum, ili kurahisisha na kuimarisha uratibu, usimamizi na utekelezaji wa afua za ustawi wa jamii nchini.

Taarifa za kuundwa kwa idara hiyo, ilitolewa jana na Waziri wa Wizara hiyo, Dk. Dorothy Gwajima, wakati akifunga mkutano wa tatu wa mwaka wa maofisa ustawi wa jamii katika Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro.

Waziri Dk. Gwajima, alisema lengo la kuanzisha idara ya ustawi wa jamii itakayojitegemea ni ongezeko la uhitaji wa huduma za ustawi wa jamii kisekta, kunako hitaji taasisi madhubuti katika kusimamia na kuratibu utoaji wa huduma hizo katika jamii kupitia taasisi za umma, binafsi na wananchi kwa ujumla.

Kwa mujibu wa Gwajima hatua hiyo ni matokeo ya kukubaliwa kwa wasilisho la mapendekezo ya haki jinai kwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema mpango huo kwa sasa unasubiri maelekezo ya muundo wa idara hiyo kupitia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Alisema: "Namshukuru sana, Rais Samia Suluhu Hassan ambaye ni Ofisa Ustawi wa Jamii namba moja, kwa kutambua mchango wa kazi zenu na kuipa kipaumbele tasnia hata kubariki tuendelee kufanya mkutano huu kila mwaka, ili kupata nafasi ya kujifunza mambo mazuri kutoka kwa wenzetu," alisema.

Kadhalika, Waziri Dk. Gwajima, alisema elimu itakayotolewa na moafisa hao itasaidia jamii kuelewa mambo mbalimbali ya huduma za kiustawi.


Alisema familia ndiyo taasisi pekee ambayo ni nguzo muhimu katika malezi bora inayomwandaa mtoto kuwa mwanaume au mwanamke bora wa baadaye na familia ndiyo mahali salama kwa watoto kukua na kufikia utimilifu wao.

Alisema: "Familia zimekuwa zikikumbwa na changamoto nyingi ikiwamo umaskini, migogoro ya ndoa na familia, malezi duni kwa watoto inayopelekea kukosekana kwa muunganiko na mahusiano hafifu kati ya wazazi au walezi na watoto wao, ambapo athari zake ni pamoja na watoto kukosa upendo wa wazazi au walezi".

Awali, Mwenyetiki wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, Fatma Tawfiq, alisema anatambua kuwa wataalam hao wamefanya tathmini ya mambo yote yanayotakiwa ili kuboresha utendaji kazi zao na kutatua changamoto zao.

Alisema kamati yake itaendelea kuishauri serikali kuongeza bajeti ili kuwawezesha maofisa ustawi jamii kutekeleza majukumu yao kwa ufasaha.

Mkutano wa tatu wa mwaka wa maofisa ustawi wa jamii, uliotanguliwa na kauli mbiu 'Tanzania bila ukatili inawezekana, imarisha uhusiano ndani ya familia' umefanyika kwa siku tatu, kuanzia Septemba 18 hadi 20 mwaka huu.



# RC Shinyanga aanika vijana wanavyotumia mikopo 'kubeti'

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Anamlinga Macha, ameeleza namna baadhi ya vikundi vya ujasiriamali vya vijana vinavyotumia mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri katika michezo ya kubahatisha.

Amesema hali hiyo inawasababishia wengi wao kushindwa kuirejesha kwa wakati.

Alisema hayo juzi mkoani hapa wakati wa uzinduzi wa Programu ya Imarisha Uchumi na Mama Samia, ambayo inasimamiwa na Ofisi ya Rais Ikulu kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC).

Programu hiyo inayahusisha makundi mbalimbali ikiwamo ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Alisema vijana wengi wanaunda vikundi na kwenda kuomba mikopo halmashauri na wanapopewa fedha wanagawana na kwenda kucheza michezo ya kubahatisha na kuacha lengo lililowawezesha.

Macha alisema kwa kuliona hilo Halmashauri ya Manispaa ya Kahama ilianzisha mpango wa kuwapatia vijana pembejeo za kilimo bure, wenye uwezo wa kulima hekari tano na kuendeleza mazao ya chakula na biashara.

Alisema wapo wanaojitokeza na kuchukua pembejeo hizo na kwenda kulima pamba, mahindi, mpunga na mazao mengine na wamenufaika kwa kubadilisha maisha yao.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2019/2020 halmashauri hiyo ilitenga Sh. milioni 54 na kila mwaka wamekuwa wakiongeza bajeti kwa sababu ya vijana kuelewa na kujitokeza.

"Nikiwa Mkuu wa Wilaya ya Kahama nimejifunza mengi kupitia vikundi vya ujasiriamali vijana, wanachukua mikopo wanagawana na kuzielekeza kwenye michezo ya kubahatisha, kurejesha inachukua muda sana, sasa Manispaa iliweka mpango wa kuwainua kupitia kilimo kwa kuwapatia pembejeo bure," alisema Macha.

Katibu Mtendaji wa NEEC, Beng'I Issa alisema hatua ya kwanza ya programu hiyo itahusisha uandaaji wa kanzi data ya walengwa, utambuzi wa shughuli zao za kiuchumi za uwezeshaji kwa vikundi vilivyotambuliwa vya wanawake, vijana pamoja na watu wenye ulemavu.

Mshauri wa Rais (Wanawake na makundi maalum), Sophia Mjema, alisema Rais Samia amewatuma kufufua majukwaa yote ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ambayo yalikuwa yamelala, kwamba ndiyo sababu wanazunguka mikoani ili kutambulisha programu hiyo kwa kukutana na viongozi na makundi yote.

Alisema tangu NEEC ilipoanzishwa mwaka 2018 wameshawafikia wananchi 11,852, kutoa mikopo ya Sh.bilioni 19.9, ushauri kwa wananchi 8,826, mafunzo kwa wananchi 11,893 pamoja na kushirikiana na kampuni 1,906 na kuwataka wananchi kuchangamkia fursa hiyo ili kujiinua



Mbunge wa Kishapu, Boniphace Butondo (mwenye shati jeupe), akiwa na baadhi ya wananchi na viongozi wa CCM, wakiangalia eneo lililochimbwa kisima cha maji ambacho atakijenga kwa kushirikiana na dada yake, Margareth Butondo ambaye anaishi Ufaransa, kwa ajili ya kusaidia wananchi wa Kijiji cha Kisesa, wilayani Kishapu. Kisima hicho hadi kukamilika kwake kitagharimu Sh. milioni 27. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Mil. 27/- zapeleka maji Kijiji cha Kisesa

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

MBUNGE wa Jimbo la Kishapu, Boniphace Butondo, pamoja na dada yake Margareth Butondo wametoa Sh.milioni 27 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maji katika Kijiji cha Kisesa wilayani hapa.

Mradi huo ni wa kisima kirefu ambao tayari umeshaanza utekelezaji kwa hatua za awali za uchimbaji na unatarajiwa kukamilika ndani ya miezi mitatu ijayo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Butondo alisema wananchi wa kijiji hicho walikuwa wanakabiliwa na tatizo la maji, hali iliyowafanya kujadilili juu ya namna ya kuwanusuru na tatizo hilo.

Alisema serikali ndani ya muda mfupi imefanya kazi kubwa katika kumtua mama ndoo kichwani nchini ikiwa ni pamoja na Jimbo la Kishapu, ambako miradi mingi ya maji imetekelezwa ili kuwaondolea adha ya maji wananchi.

Vilevile alisema tayari serikali imetoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa ujenzi wa visima vitano vya maji kwa kila jimbo ili kuhakikisha kila mwananchi anafikiwa na huduma ya majisafi na salama.

"Kutokana na juhudi hizi ambazo zinafanywa na serikali kutatua changamoto ya ukosefu wa maji na kumtua ndoo kichwani mwanamke, ndipo mimi na dada yangu tukaona tumuunge mkono Rais Samia na kutoa fedha zetu binafsi kuanzisha ujenzi wa mradi wa maji wa kisima kirefu katika kijiji hiki," alisema.

Fundi kutoka RUWASA wilayani Kishapu, Alex Makono, alisema watashirikiana na familia hiyo kwa kila hatua hadi kukamilisha mradi huo ikiwamo kusambaza maji katika kila kitongoji baada ya kujengwa kwa tangi kubwa.

Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Kisesa walisema hali ya upatikanaji maji kijijini hapo ni ngumu hali inayowalazimu kutumia maji machafu.

Walisema kukamilika kwa mradi huo kutawasaidia kutatua shida hiyo na kuondokana na matumizi ya maji yasiyo safi na salama.

# Mjema awataka Ma-RC, DC kuibua fursa kiuchumi

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

MSHAURI wa Rais (wanawake na makundi maalum), Sophia Mjema, amewaagiza wakuu wa mikoa na wilaya nchini kuibua fursa za kiuchumi kwenye maeneo yao kwa kuainisha kipaumbele kwa fursa zilizopo, ili kuleta maendeleo kwa makundi yote.

Alitoa agizo hilo wakati wa kikao maalum cha mpango wa kuimarisha uchumi kilichofanyika mkoani Geita, kuratibiwa na Ofisi ya Rais Ikulu kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi kiuchumi (NEEC).

Alisema kuwa wakuu hao ni vyema wakaibua fursa za kiuchumi ili kuweka kipaumbele kwa kila mkoa, lengo likiwa ni kuhakikisha makundi hayo yanaondokana na umaskini.

Alisema kuwa mpango huo ni maono ya Rais Samia Suluhu Hassan ukilenga kuhuisha majukwaa na kuyatambua kwa idadi kuanzia ngazi ya kata, wilaya na mkoa ili kuwainua wananchi kiuchumi kutoka kwenye wimbi la umaskini kwa vijana, wanawake na walemavu.

"Mpango huu ni kwa mikoa 26 ya Tanzania Bara na mikoa mitano kwa Zanzibar na ili mkoa ufanikiwe kiuchumi ni lazima uwepo mpago uliopewa kipaumbele mfano katika sekta ya kilimo, uvuvi, ufugaji na uchimbaji madini," alisema Mjema.

Katibu Mkuu Mtendaji wa NEEC, Beng'i Issa alisema wananchi wengi hawana uwezo wa kushiriki kwenye sekta ya fedha kwa kutokuwa na mitaji na kutosajiliwa.

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martine Shigela alisema kuwa katika mkoa huo zipo fursa mbalimbali za kilimo, ufugaji, uvuvi na uchimbaji madini ya dhahabu.

**"Mpango huu ni kwa mikoa 26 ya Tanzania Bara na mikoa mitano kwa Zanzibar na ili mkoa ufanikiwe kiuchumi ni lazima uwepo mpago uliopewa…**

NIPASHE SEPTEMBA 23, 2024
Nipashe
Spotika




MECHI ZA KWANZA MUUNDO MPYA UEFA NA UBORA WAKE UK. 12-13




# YILDIZ ANAVYOONEKANA DEL PIERO MPYA JUVENTUS

**TURIN,** Italia

WAKATI Kenan Yildiz alipouchukua mpira kutoka upande wa kushoto, akakimbia mbele, akapinda bega na kumpita beki wa PSV Eindhoven, na kisha kujipinda kwa shuti lililojaa kona ya juu kabisa ya wavu, kila shabiki wa Juventus aliyehudhuria kwenye Uwanja wa Allianz au aliyekuwa nyumbani kwenye sofa alisimama na kupiga kelele: "Del Pieroooo!"

Na ingawa hii ilikuwa imefanywa na Freudian, liilikuwa ni jambo la kueleweka sana kwa mashabiki.

Kwanza, bao hilo lilifungwa na mchezaji aliyevalia jezi namba kumi ya Juve - na lilifanana kila kitu na alilowahi kufunga nyota na gwiji wa klabu hiyo, Alessandro Del Piero.

Mitandao ya kijamii iliweka video ya kufananisha bao maarufu la Del Piero dhidi ya Steaua Bucharest.

Yildiz alicheza katika ulinganisho uliotarajiwa pia, akinyoosha ulimi wake katika kushangilia kama vile Del Piero alivyokuwa anafanya baada ya mabao yake yote 290 akiwa na 'Kibibi Kizee' hicho cha Turin.

Ulinganisho kati ya namba 10 mpya wa Juventus na namba kumi bora wa wakati wote wa klabu hiyo uliwaweka vijana wa Thiago Motta kwenye njia yao ya kushinda mabao 3-1 dhidi ya PSV.

Tangu siku ya kwanza alipowasili Juve kutoka Bayern Munich akiwa na umri wa miaka 17, kinda huyo wa Kituruki amekuwa akitajwa kuwa 'Del Piero anayefuata'.

Imekuwa bili ambayo imekuwa na uzito mkubwa kwa watu wanaojidai kushika kiti cha enzi hapo awali. Sebastian Giovinco, ingawa alikuwa na kazi nzuri, hakuwahi kufikia kiwango cha Del Piero ambacho mashabiki wa Juve walitarajia angeweza.

Wala haikufaa kabisa kwa wahitimu wa akademia Davide Lanzafame, au Filippo Boniperti. Na kutokana na majeraha yaliyokuwa yakizidi kuwaathiri, Paulo Dybala na Federico Chiesa hawakuwahi kufika hata kwenye hadhi ya kuwa magwiji wa Juventus.

Wakati huu, mambo yanaonekana kuwa tofauti kwa Yildiz. Namna klabu inavyoweka msisitizo kwa chipukizi huyo ni dalili tosha kufanikisha hilo.

Baada ya kustaajabisha kwa kupewa dakika za hapa na pale chini ya kocha wa awali Massimiliano Allegri msimu uliopita, mkataba mpya wa muda mrefu na jezi namba 10 ni ishara kwamba uongozi wa klabu hiyo umepania kujenga kikosi chao kipya karibu na mchezaji huyo wa Kimataifa wa Uturuki - licha ya yeye kuwa na umri wa miaka 19 tu.

Na hadi sasa, hiyo inaonekana kama ni uamuzi wa busara. Yildiz amefanikiwa katika jukumu hili jipya kama nyota wa klabu, akicheza, anayetakiwa kuibeba timu kama alivyokuwa akifanya Del Piero.

Uthibitisho wa hilo unaweza kupatikana katika ukweli kwamba tayari anavunja baadhi ya rekodi za muda mrefu za Del Piero katika klabu hiyo - hivi majuzi akiwa mchezaji mdogo zaidi wa Juve kuwahi kuanza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na mfungaji mabao katika ushindi dhidi ya PSV Eindhoven.

Inaweza pia kupatikana katika viwango vyake vya uchezaji katika Serie A katika wiki chache za kwanza za msimu wa 2024/25.

Wakati bado hajafunga bao la ligi, namba kumi amekuwa kitovu cha kila safu ya ushambuliaji ya Juve, mara kwa mara akiwapita wachezaji wa timu pinzani na kuwalisha mpira wachezaji wenzake kwenye maeneo hatari - huku asisti zake mbili katika mechi nne zikihusika.

Atakapopata bao kwenye Serie A, inatarajiwa mashabiki wa Juve wasimame tena na kusema: "Del Pieroooo!"


Kwa mshangao wa "Del Pieroooo!" wakati wowote Yildiz anapofunga watakuwa mashabiki wa Juve wakipiga kelele "Lisan Al Gaib!", wakimsifu Yildiz kama ujio wa pili wa mchezaji wao bora zaidi.

## ISIKUPITE

BAO alilofunga Harry Kane juzi wakati Bayern Munich ikishinda 5-0 dhidi ya Werder Bremen linamfanya kuwa mchezaji wa kwanza kutoka England kufikisha mabao 41 katika historia ya Bundesliga, akiipiku rekodi iliyokuwa ikishikiliwa na Jadon Sancho, ambaye alifunga mabao 40 katika ligi hiyo akiichezea Borussia Dortmund.



# MECHI ZA KWANZA MUUNDO MPYA UEFA NA UBORA WAKE



RAYA

**PARIS,**
Ufaransa

RAUNDI ya kwanza ya mechi za Ligi ya Mabingwa Ulaya imekamilika na sasa tunajaribu kuangalia namna mambo yalivyokuwa.

**Muundo ni mpya msimu huu huku timu zikiwa zimeongezeka hadi 36 badala ya 32 zilizokuwa zinagawanywa kwa makundi nane.**

BBC Sport inaangalia kile kilichotokea katika mzunguko wa kwanza wa michezo na jinsi ushindani ulioboreshwa unavyoonekana.

### # Msimamo mpya wa ligi

Awamu hii mpya badala ya timu kuuunda makundi nane yenye timu nne, imekuwa tofauti na itachukua muda kuzoea.

Msimamo mmoja mkubwa wenye timu 36 ni jambo ambalo hatulioni hata kwenye soka la ligi za nchi mbalimbali.

Kumbuka, timu zitakazomaliza katika nafasi nane za juu zitafuzu moja kwa moja kwa hatua ya 16 bora, huku zile zitakazoshika nafasi ya tisa hadi 24 zitachuana katika hatua ya mtoano kwa mikondo miwili ili kupata nafasi ya kuungana nazo.

Yeyote atakayemaliza nafasi ya 25 au chini ataondolewa. Kwa hiyo ni theluthi moja tu ya timu hutoka baada ya kila mtu kucheza mechi nane.

Kwa mujibu wa Opta, pointi 16 kutoka mechi 24 zinazowezekana zinatoa nafasi ya asilimia 98 ya kumaliza nane bora.

Pointi 10 ni asilimia 99 ya uwezekano wa kumaliza nafasi ya 24 bora, kwa hiyo timu zilizoshinda wiki hii zinahitaji ushindi mara mbili tu na sare moja ili kupata nafasi ya kutinga hatua ya 16-bora.

Timu 15 zilishinda michezo yao ya ufunguzi (ikimaanisha timu 15 zilipoteza) ambayo inaacha klabu sita katikati kwa alama moja.

Kwa kifupi, ukishinda una nafasi kubwa ya kupita. Ikiwa umepoteza ... bado una nafasi nzuri.

### # Ilikuwa ya ushindani?

Ni mapema mno kusoma mpangilio wa matokeo... lakini vinara wa juu walipoteza pointi zaidi wakati huu ikilinganishwa na mzunguko wa kwanza wa michezo ya kundi mwaka jana.

Msimu uliopita timu sita kubwa kati ya nane zilishinda, huku moja ikitoka sare na kupoteza mmoja.

Mwaka huu kulikuwa na vinara tisa wa juu, huku watano wakishinda, wawili wakitoka sare na wawili wakipoteza.

### # Timu za chini zilifanya vizuri zaidi

Timu nne cha chini kati ya tisa kwenye 'chungu cha nne' zilishinda - ikiwa ni pamoja na Aston Villa. Mwaka jana hakuna timu yoyote kati ya nane za chini iliyoshinda mchezo wao wa kwanza wa kundi.

### # Michezo mikubwa ilileta matokeo?

Moja ya faida za muundo mpya ni michezo zaidi kati ya timu kubwa.

Tofauti na siku za nyuma, kila timu kubwa ya juu itakutana na timu nyingine mbili kutoka chungu cha juu pia.

Mechi pekee kubwa ilikuwa Manchester City dhidi ya Inter Milan... ambayo iliisha kwa sare ya bila kufungana.

Lakini hiyo haikuwa mechi pekee iliyovutia macho katika mzunguko wa kwanza, Liverpool ikikutana na AC Milan katika marudio ya fainali za 2005 na 2007. Timu hiyo ya Ligi Kuu England ilishinda 3-1.

Mechi kubwa zinazokuja hivi karibuni, si lazima ziwe kubwa zaidi, ni Arsenal dhidi ya Paris St-Germain katika kundi lijalo la michezo, pamoja na Real Madrid dhidi ya Borussia Dortmund - ambayo ni kama marudio ya fainali ya mwaka jana.

Barcelona dhidi ya Bayern Munich iko katika raundi ifuatayo ya ratiba - ingawa wawili hao walikutana katika hatua ya makundi miaka miwili iliyopita.

### # Timu za Uingereza vipi

Ulikuwa ufunguzi mzuri kwa timu tano za Uingereza katika Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa tatu kushinda na mbili kupata sare.

Celtic iliishinda Slovan Bratislava mabao 5-1, Aston Villa ikailaza Young Boys 3-0 na Liverpool ikashinda 3-1 dhidi ya AC Milan.

Manchester City na Arsenal zote zilitoka sare tasa na timu za Italia, mabingwa wa Serie A, Inter Milan na washindi wa Ligi ya Europa Atalanta.

### # Wachezaji waliovutia macho

Harry Kane aliifungia Bayern Munich mabao manne walipoichabanga Dinamo Zagreb 9-2. Hiyo tayari imempeleka kufikia nusu ya jumla ya mabao yaliyomfanya kushinda kiatu cha dhahabu msimu uliopita.

Wachezaji wengine watatu walifunga mabao mawili, yote kwa klabu za Ujerumani - winga wa Borussia Dortmund na England chini ya umri wa miaka 21, Jamie Gittens, Michael Olise wa Bayern Munich na Florian Wirtz wa Bayer Leverkusen.

Golikipa aliyekuwa na matokeo ya kukumbukwa katika raundi ya kwanza ya mechi alikuwa David Raya wa Arsenal, ambaye alifanya kazi nzuri ya kuokoa mara mbili - ikiwa ni pamoja na mkwaju wa penalti - na kumnyima bao mshambuliaji wa Atalanta, Mateo Retegui.

### # Timu zitakazoshangaza

Timu ambazo zinaweza kuwa na furaha zaidi na kazi yao ni Celtic, ambayo ilifunga mabao matano katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa kwa mara ya kwanza, na Sparta Prague.

Sparta, katika mchezo wao wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa kwa miaka 19, waliifunga Salzburg 3-0.

Brest ya Ufaransa, ambayo ilikuwa ikicheza mechi yake ya kwanza katika mashindano yoyote ya Ulaya, ilishinda Sturm Graz 2-1.

Girona, ambayo pia alicheza mechi ya Ulaya kwa mara ya kwanza, walikuwa sekunde chache kutoka sare huko Paris St-Germain kabla ya Paulo Gazzaniga kujifunga.

## Nukuu

"[Kylian] Mbappe anaonekana mchanga zaidi, akifanya kazi zaidi kwenye mpira, ni hatari sana, ukichanganya vema na Vinicius na washambuliaji wengine, anaimarika," **Kocha wa Real Madrid, Carlo Ancelotti**



"Nimesikia uvumi tayari kutoka kwa wachambuzi. Ni wazimu, kama mtu hauko sawa unapoleta uvumi kama huo wakati haujui, ilikuwa ni mzunguko tu. Nina furaha sana na Marcus katika kila kitu anachofanya," **Kocha wa Manchester United, Erik ten Hag akiwajibu wachambuzi kuhusu uvumi kwamba uamuzi wake wa kumweka benchi Marcus Rashford dhidi ya Crystal Palace Jumamosi.**



"Sikufurahia maandalizi kwa sababu sikulala sana, nilitayarisha mikutano yote, vipindi vya mazoezi na kila kitu. Kisha nikapata habari kwamba tumepoteza mchezaji, na kisha mchezaji mwingine na mchezaji mwingine, ikabidi nibadilishe kabisa na kurekebisha mpango kwa wachezaji, tulikuwa na fursa kwa hiyo, ilikuwa ni changamoto kubwa," **Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, kabla ya kuivaa Spurs na kushinda bao 1-0.**





Wachezaji wa Azam FC, wakishangilia moja ya mabao yao manne waliyofunga katika mchezo wao dhidi ya KMC , uliopigwa Uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam, Alhamisi iliyopita, ikiwa ni moja kati ya michezo miwili iliyotoa vipigo vikubwa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa.

# TAKWIMU, REKODI 10 ZA MABAO LIGI BARA

**Na Adam Fungamwango**

JUMLA ya mabao 53 yalikuwa yamefungwa kwenye michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka kufikia juzi, Jumamosi.

Mabao hayo yamefunga na wachezaji 40 katika michezo 30 ambayo imechezwa mpaka sasa. Tayari Ligi Kuu Tanzania Bara imeshaingia raundi ya tano kwa baadhi ya timu, lakini zingine bado hazijacheza hata raundi mbili, ikiwamo Yanga.

**Kwenye makala haya, tunakuletea aina na staili ya mabao hayo 53 yaliyofungwa mpaka sasa, huku pia wakiwamo timu na wachezaji waliweka rekodi ya mabao hayo, twende sasa...**

### 1# Mabao matatu ndani ya sekunde chache

Jumla ya mabao matatu yamefungwa kabla dakika moja haijakamilika. Septemba 12, Paul Peter wa Dodoma Jiji alifunga bao sekunde ya 39, wakati timu yake ikiichapa Namungo bao 1-0, Uwanja wa Tanzanite Kwaraa, Septemba 17, Emmanuel Keyekeh wa Singida Black Stars, naye alipachika mabao sekunde ya 20, likiwa ni bao pekee, timu yake ikiichapa Pamba Jiji 1-0, Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza, na Septemba 20, mwaka huu, Peter Lwasa akiifungia Kagera Sugar bao sekunde ya 51, ikishinda nyumbani, Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera.

### 2# Mabao 32 ya mguu wa kulia

Mabao 32 yamefungwa kwa mguu wa kulia mpaka sasa, huku Fountain Gate ikiongoza kwa wachezaji wake kupachika mabao kwa mguu huo.

Kati ya mabao tisa ambayo wamefunga mpaka sasa, manane yakifungwa kwa mguu wa kulia, wakifuatiwa na timu ya Simba na Singida Black Stars ambazo wachezaji wao wamefunga mabao sita kila moja kwa kutumia mguu huo.

### 3# Mabao 14 ya mguu wa kushoto

Wakati mabao 14 yakiwa yamefungwa kwa mguu wa kushoto kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa, Tabora United ndiyo inayoongoza kwa kupachika mabao mengi kwa kutumia mguu huo.

Wachezaji waliofanya hivyo mpaka sasa, ni Heritier Makambo, Shedrack Asiegbu na Yacouba Songne, ambao wameifanya kuwa na mabao matatu ya mguu wa kushoto, huku KMC ikifuatiwa ikiwa imepachika mabao mawili kwa kutumia mguu huo, kupitia kwa mchezaji wake Redemtus Mussa, aliyefunga mabao yote hayo.

### 4# Mabao saba ya vichwa

Mabao saba yamefungwa kwa vichwa mpaka sasa, huku Simba na Singida Black Stars ndizo zinaongoza kila timu ikipachika mabao matatu kwa njia hiyo.

Straika wa Singida Black Stars, Elvis Rupia, anaongoza kwa kufunga mabao mawili peke yake kwa njia hiyo na kuwa mchezaji kinara kwenye Ligi Kuu mpaka sasa kufungwa kwa vichwa. Mchezaji mwingine wa Singida ni Mohamed Damaro.

Kwa upande wa Simba, Che Fondoh Malone, Edwin Balua na Valentine Mashaka, wamefunga mabao hayo kwa njia hiyo katika michezo miwili ambayo timu hiyo imecheza mpaka sasa.

### 5# Mabao 44 ndani ya boksi

Kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa jumla ya mabao 44 yamefungwa ndani ya eneo la hatari na wachezaji mbalimbali, huku wa Fountain Gate wakionekana makini sana wakiwa ndani ya boksi.

Timu hiyo imefunga mabao manane ambayo wachezaji wake wakiwa ndani ya boksi na kuwa timu inayoongoza kwa kufunga mabao wakiwa karibu na lango.

### 6# Mabao tisa nje ya boksi

Yamefungwa mabao tisa nje ya eneo la hatari mpaka sasa, na KMC ndio wanaoongoza kwa kupachika mabao mawili wakiwa nje ya boksi.

Na aliyewafanya kuweka rekodi hiyo mpaka sasa ni mchezaji wao, Redemtus Mussa, ambaye amefunga mabao yote akiwa nje.

Kumbuka mchezaji huyu ndiyo aliyefunga mabao mawili kwa mguu wa kushoto, akiifanya timu yake kuwa ya pili, yote aliyafunga nje ya boksi.

### 7# Mabao matano ya penalti

Kati ya mabao 53 yaliyofungwa, mabao matano yamefungwa kwa mikwaju ya penalti. Jumla ya penalti nane zimetolewa na waamuzi, lakini tano ndiyo zilizotinga nyavuni na tatu zikaota mbawa.

Wachezaji ambao wamepachika mabao kwa mikwaju ya penalti mpaka sasa ni Djuma Shaaban wa Namungo, Makambo na Asiegbu, wote wa Tabora United, Ibrahim Elias wa KMC na Salum Kihimbwa wa Fountain Gate.

### 8# Bao moja la kujifunga

Kuna bao moja tu la kujifunga mpaka sasa, na lilipatikana Septemba 19, mwaka huu, Uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam, ambapo Fred Tangalo wa KMC aliuweka mwenyewe mpira wavuni katika harakati za kuokoa timu yake ilipocheza dhidi ya Azam FC na kupoteza kwa mabao 4-0.

### 9# Mechi mbili za vipigo vikali

Ni michezo miwili tu ambayo imetoa vipigo vikali zaidi mpaka sasa. Michezo hiyo ni ile ambayo Simba iliichakaza Fountain Gate mabao 4-0, mchezo ukichezwa, Agosti 25, Uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam, na ule uliopigwa, Septemba 19, Azam ikiibamiza KMC mabao 4-0 kwenye uwanja huo huo.

### 10# Mabao ya faulo

Mpaka sasa ni mabao mawili tu yaliyofungwa kwa faulo ya moja kwa moja. Wachezaji waliopachika mabao kwa njia hiyo ni Dickson Ambundo wa Fountain Gate na Redemtus wa KMC.

Ambundo alifanya hivyo, Septemba 15, akipopiga faulo iliyokwenda moja kwa moja wavuni, akiiandikia timu yake bao la pili la kusawazisha, Uwanja wa Tanzanite Kwaraa, Babati, Manyara, dhidi ya Dodoma jiji na kumalizika kwa sare ya 2-2, na kwenye Uwanja wa KMC Complex, Redemtus alifunga kwa mkwaju wa faulo na kuipatia bao pekee katika mchezo dhidi ya KenGold, Septemba 16, mwaka huu.

## JE, WAJUA?




KIPA wa Arsenal, David Raya, ndiye golikipa aliyekuwa na matokeo ya kukumbukwa zaidi katika raundi ya kwanza ya mechi za Ligi ya Mabingwa Ulaya, baada ya kufanya kazi nzuri ya kuokoa mara mbili - ikiwa ni pamoja na mkwaju wa penalti – na kumnyima bao mshambuliaji wa Atalanta, Mateo Retegui.



# DC apiga marufuku vikundi vya 'Nkili'

**Na Thobias Mwanakatwe,** IRAMBA

MKUU wa Wilaya ya Iramba mkoani Singida, Suleiman Mwenda, amepiga marufuku vikundi vinavyojulikana kama 'Nkili' ambavyo vimeweka utaratibu wa kutoza faini ya ng'ombe, mbuzi na fedha wananchi kwa kuwa vitendo hivyo havizingatii taratibu na sheria za nchi.

Mwenda alipiga marufuku hiyo juzi alipokuwa akizungumza katika mkutano wa hadhara na wananchi wa Kijiji cha Kinalilya baada ya mwananchi Wilfred Tuntuma kulalamika kutozwa faini ya ng'ombe watatu na kikundi hicho ambacho kimekuwa kikifanya hivyo kwa wanakijiji kila mara.

Wiki iliyopita gazeti hili liliandika taarifa kuhusu uwepo wa vikundi vya nkili katika vijiji vinne vya Kata ya Kisiriri na kata nyingine katika wilayani Iramba ambavyo vinatoza faini hizo wananchi na asiyetoa hutengwa katika shughuli za kijami.

"Kuanzia sasa ni marufuku katika wilaya hii utaratibu wa kuwekeana faini bila kufuata utaratibu, bila kuzingatia viwango, haiwezekani mkawa mnatozana faini ambazo zinakinzana na sheria za nchi," alisema.

Mwenda alisema utaratibu wa kutozana faini unaowekwa kwenye vitongoji na vijiji hautakiwi na unakinzana na sheria za nchi.

"Kwa suala la mzee Wilfred Shalua Tuntuma kulipishwa ng'ombe wakati mahakama ilishasema hahusiki na tukio lililotokea kijijini kwenu sasa nyie mnamhukumu kwa jambo lipi na mahakama na polisi wana wataalamu waliosomea kuhoji na kuchunguza kujua nini kimefanyika hapa," alisema.

Mwenda alisema wananchi lazima watambue kuwa kila mtu ana haki ya kuishi, kuheshimiwa na kuhakikishiwa usalama katika makazi yake anayoishi.

**"Kuanzia sasa ni marufuku katika wilaya hii utaratibu wa kuwekeana faini bila kufuata utaratibu, bila kuzingatia viwango, haiwezekani mkawa mnatozana faini ambazo zinakinzana na sheria za nchi," alisema.**

# Mchengerwa kula sahani moja watakaohujumu mikopo 10%

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, amesema hatasita kuwachukulia hatua watendaji watakaobainika kuhujumu au kufanya ubadhirifu wa fedha za mikopo ya asilimia 10 zinazotolewa na halmashauri.

Alisema hayo jana jijini hapa alipokuwa akifunga mafunzo ya wasimamizi wa mikopo hiyo wakiwamo maofisa maendeleo ya jamii, wasimamizi wa fedha, waratibu wa mikopo, wahasibu na maofisa Tehama wa mikoa na wilaya.

Alisema wasimamizi wa mikopo hiyo wanapaswa kuratibu utoaji wake kwa uzalendo ili iwanufaishe walengwa na iwe na tija kwa jamii na taifa kwa malengo yaliyokusudiwa na serikali.

Alieleza kuwa hadi kufikia mwaka 2024/25 fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya mikopo hiyo tangu utoaji wake uliposimamishwa ni zaidi ya Sh.bilioni 160.

Mchengerwa alisema fedha hizo zitatumika kutoa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

"Mikopo hii inatolewa na serikali kwa ajili ya kuwawezesha kiuchumi wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili waweze kujikomboa kiuchumi kwa kufanya shughuli mbalimbali za ujasiriamali, hivyo sitosita kuwachukulia hatua watakaokwamisha makundi lengwa kupata mikopo," alisema.

Mchengerwa alisema mikopo hiyo ikisimamiwa vizuri na kuwafikia walengwa itabadilisha maisha ya wanufaika hao na kuwataka wasimamizi hao kutoa elimu ya namna bora ya kuitumia mikopo hiyo kuboresha maisha yao na kufanya marejesho kwa wakati ili kuwezesha wengine kunufaika.



Baadhi ya wafanyabiashara wa mifugo wakiwa kwenye Mnada wa Mifugo Kigwe, Halmashauri ya Wilaya ya Bahi, mkoani Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Machifu wasisitiza amani, 'kumsapoti' Rais Samia

**Na Mwandishi Wetu**

MACHIFU nchini wamewaomba Watanzania kulinda amani iliyopo na kutokubali kuyumbishwa na watu wanaobeza jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan za kuwaletea maendeleo.

Aidha, wamemshukuru Rais Samia kwa kutambua umuhimu wao na kuahidi kuendelea kuombea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika mwaka huu na Uchaguzi Mkuu ili Tanzania iendelee kuwa na amani.

Akizungumza jana mjini Songea kwenye mjadala wa mstakabali wa Tanzania kwenye masuala ya mila na desturi ikiwa ni maadhimisho ya Tamasha la Tatu la Kitaifa la Utamaduni, Mwenyekiti wa Machifu Tanzania, Chifu Antonia Matalu, alisema wamejadili masuala mbalimbali ikiwamo namna Rais Samia anavyowajali na kutambua umuhimu wao kwa jamii na kukemea Watanzania wanaomdharau na kutishia kufanya maandamano.

"Machifu tutamlinda Rais Samia kwa gharama yoyote kwa sababu tunampenda, amehimiza mila na tamaduni zetu kuheshimiana, Rais Samia ni zawadi kwetu," alisema.

Alisema Rais Samia amewapa majukumu ya kushikamana na raia kwa maendeleo ya Tanzania.

"Tunamwamini mama (Rais Samia) ni jasiri na tunaimani naye nchi hii anaiendesha vizuri, hapa machifu tumezungumzia maadili Rais Samia aheshimiwe na tunakemea wale wanamdharau waache mara moja," alisema.

Alisema machifu wanapenda amani na wanasisitiza Watanzania wailinde na kuitunza.

Alisema: "Tumeshuhudia nchi nyingi zikipigana na sisi tukipokea wakimbizi, sisi tuna Rais mama mwenye huruma hata wale waliokimbia aliwaambia warudi watoto wangu mrudi nyumbani mnataka nini, tumpe mama yetu amani, msaada viongozi wote tushikamane naye kumpa faraja maana anatukanwa kwa ajili ya Watanzania".

Alisema Tanzania ni tulivu na siyo watu wa maandamano na nchi zingine zimekuwa zikitamani amani iliyopo.

"Sisi sio watu wa maandamano hata kidogo, tunaomba Rais Samia Suluhu Hassan aheshimiwe, machifu hapa tunasema Rais aheshimiwe," alisema.

Naye Dada wa Chifu Adam II, Fatma Mkwawa alisema: "Tuombee uchaguzi na Rais wetu Samia Suluhu Hassan aendelee kutuongoza kwa kuwa mama halali kwa ajili yetu, tutamuombea. Niwaombe viongozi wa kimila ambao ni vijana mpate muda wa kuzungumza na vijana wenzenu."

Aidha, alisema suala la maadili linapaswa kufuatiliwa kwa karibu na viongozi wa kimila na kutoa msaada kwenye makuzi ya watoto hasa wanaojilea wenyewe bila wazazi.

Alihimiza vijana kutunza amani, mila na desturi na kujiepusha na mapenzi ya jinsia moja ili Tanzania iendelee kupiga hatua za kimaendeleo

Chifu Songea Mbano 1, Samweli alimshukuru Rais Samia kwa kazi kubwa ambayo anaifanya ya kushirikisha viongozi wa kimila na kuomba elimu iendelee kutolewa ili vijana watambue machifu siyo wachawi bali ni watu wa mila na desturi.





# Polisi yaendesha operesheni kamata 'mikweche'

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SIKU chache baada ya kutokea ajali iliyoua watu zaidi ya 20 na kujeruhi wengine mkoani Mbeya, Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani limeanza kufanya operesheni maalumu ya kukagua magari ya abiria na kuchukua hatua za kishera.

Kati ya ajali hizo zilizotokea mkoani humo, mojawapo ilitokea katika Kata ya Lwanjilo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ambayo ililihusisha basi la Kampuni ya AN CLASSIC lililokuwa likifanya safari zake kati ya Jiji la Mbeya na Mkoa wa Tabora ambalo lilianguka na kusababisha vifo vya watu 12 na kujeruhi 33.

Operesheni ya ukaguzi wa magari hayo ilianza juzi wilayani Chunya ambapo iliongozwa na Mkuu wa Operesheni wa kikosi hicho, Kamishna Msaidizi wa Polisi (ACP) Nassoro Sisiowaya.

Kwenye ukaguzi wa magari hayo mabasi matatu ya abiria yalibainika kuwa na kasoro mbalimbali ambazo zinahatarisha maisha ya abiria ikiwemo ubovu kwenye mfumo wa breki.

Kamishna Sisiowaya alisema mabasi hayo yalikuwa yanafanya safari zake kati ya Jiji la Mbeya na Wilaya ya Chunya na mengine yalikuwa yanaelekea mkoani Tabora.

Alisema moja kati ya hatua walizochukua ni pamoja na kuwatoza faini madereva, kuamuru abiria washushwe na kutafutiwa magari mengine na baadhi kuamuriwa warejeshe nauli walizokuwa wamekusanya kwa abiria.

Alisema: "Operesheni hii itaendelea katika maeneo yote nchini ili kuhakikisha mabasi yanayobeba abiria ni yale tu ambayo hayana matatizo, wamiliki wa mabasi mabovu wahakikishe wanayaondoa barabarani ili waepuke adhabu".

# Nishati chafu ya kupikia yaua watu 2,750 kwa mwezi nchini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATU 33,000 wanafariki dunia kila mwaka nchini kutokana na magonjwa ya mfumo wa upumuaji ambayo yanasababishwa na uchafuzi wa mazingira pamoja na matumizi ya nishati chafu ya kupikia.

Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Christina Mndeme aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini Mbeya kwenye mkutano wa kuhamasisha matumizi ya nishati safi na uhifadhi wa mazingira.

Mkutano huo uliwashirikisha wadau mbalimbali wa mazingira wakiwamo viongozi wa dini, mama lishe na baba lishe, wasambazaji wa nishati safi (gesi), madereva bodaboda na viongozi wa madawati ya nishati safi wa halmashauri zote za Mkoa wa Mbeya.

Mndeme alisema mbali na nishati hiyo kusababisha vifo pia husababisha madhara kwa wajawazito ikiwamo mimba kutoka, kujifungua kabla ya wakati, matatizo ya uti wa mgongo, maumivu ya kichwa na kikohozi cha mara kwa mara.

Vilevile alisema nishati chafu husababisha macho kuwa mekundu na hivyo kuanza kuhusishwa na imani za kishirikina hasa kuonekana kuwa ni wachawi.

Hivyo, aliwataka wananchi kubadili tabia kwa kuanza kutumia nishati safi ya kupikia ikiwamo gesi, umeme na majiko banifu na kuondokana na matumizi ya kuni na mkaa ambazo ni nishati zinazochangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa mazingira.

Alisema kwa sasa serikali imeshatoa mwongozo maalumu unaozitaka taasisi zinazoandaa chakula na kulisha zaidi ya watu 100 kuacha matumizi ya nishati isiyo safi na kuingia kwenye matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kulinda mazingira.

Alisema Jeshi la Magereza ni miongoni mwa taasisi ambazo zimekuwa zikiongoza nchini kwa kukata miti kwa ajili ya kuni za kupikia na hivyo akalitaka kuachana na matumizi ya nishati hiyo. Kamishna kutoka Wizara ya Nishati, Stayden Rwebangira, alisema wizara imeanza mkakati wa kupunguza gharama za kujaza gesi ili kuifanya ipatikane kwa bei ambayo wananchi wote watakuwa na uwezo wa kuimudu na hivyo akawataka wananchi kuwa wavumilivu.

Alisema kwa sasa wako katika hatua za kuanzisha mfuko wa nishati safi utakaowezesha upatikanaji wa nishati hiyo kwa bei nafuu na rafiki kwa wananchi wa hali zote kiuchumi.

Hivyo, aliwataka kuchangamkia fursa za kiuchumi zinazopatikana kwenye mnyororo wa matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa maelezo kuwa kupitia mkakati huo watasogeza huduma za vituo vya ujazaji gesi hadi maeneo ya vijijini.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Felista Mdemu aliwataka wanawake mkoani Mbeya kuipokea kampeni hiyo kwa maelezo kuwa wao ndio waathirika wakuu.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa alisema mkoa huo unakabiliwa na mabadiliko ya tabianchi yanayotokana na ukataji ovyo wa miti na hivyo kampeni hiyo imekuja wakati sahihi.



Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Christina Mndeme, akizungumza na wadau mbalimbali wa mazingira kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia mwishoni mwa wiki, wakati wa mkutano wa kuhamasisha matumizi ya nishati hiyo jijini Mbeya. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Waeleza faida ujenzi Chuo Kikuu Njombe

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAKAZI wa Halmashauri ya Mji wa Njombe, wamesema ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) Kampasi ya Njombe, utasaidia kuchochea ukuaji wa uchumi katika mji huo.

Ujenzi wa chuo hicho unatarajiwa kugharimu zaidi ya Sh. bilioni 20 na eneo lenye ukubwa wa ekari 112 limetengwa kwa ajili ya mradi huo.

Chuo hicho kitakapokamilika kitaanza na wanafunzi 1,000 wa programu za stashahada katika sekta za kilimo, uvunaji wa misitu na mazao yake, uvuvi na sayansi na teknolojia.

Waliyasema hayo juzi walipozungumza na Nipashe ambapo walisema ujio wa chuo hicho ni fursa kwao wakisema kitasaidia kuchangamsha biashara zao na kuwapunguzia watoto wao umbali wa kwenda kusoma vyuo mikoa mingine.

Lucy Chaula alisema ujio wa chuo hicho ni neema kwa sababu watafanya biashara mbalimbali ikiwamo zinazotokana na mazao ya kilimo.

Michael Sanga alisema uchumi wao utakuwa kwa sababu watapangisha nyumba za kuishi na kulala wageni, watauza chakula pamoja na biashara nyingine ndogondogo.

Awali Naibu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), (Taaluma), Prof. Razack Lokina, alisema wanafunzi 1,000 wanatarajia kuanza kupata masomo ya stashahada na chache shahada.

Alisema tayari wameshatangaza zabuni ya kusaka mkandarasi wa ujenzi na wanatarajia ndani ya miezi miwili atakuwa amepatikana na kuanza kazi.

Katibu Tawala Mkoa wa Njombe, Judica Omary, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa chuo hicho kwa kuwa ni mara ya kwanza kwa mkoa huo kujengwa chuo hicho.

Mbunge wa Njombe Mjini, Deo Mwanyika aliwataka wananchi mkoani Njombe kutumia fursa ya ujenzi wa chuo hicho kupata elimu lakini kuinuka kiuchumi kutoka na ujio wa wageni chuoni hapo.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alifanya ziara katika eneo la ujenzi wa chuo hicho ambapo alisema ombi la ujenzi wa chuo kikuu mkoani Njombe limekamilika na tayari fedha zimeshatengwa na ifikapo mwaka 2026 wataanza kupokea wanafunzi.

Hata hivyo aliwashukuru wabunge wa Mkoa wa Njombe kwa jitihada za kupigania ujenzi wa chuo hicho kwa kuwa wananchi wa mkoa huo wanapenda elimu.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Njombe, Dk. Jabil Juma, alisema chuo kitakapoanza kujengwa vijana watapata ajira kwenye kutengeneza miundombinu ya chuo.

Alisema halmashauri itapata mapato ya ndani kupitia ushuru wa huduma yataongezeka kwa kuanzisha biashara mpya na kuongeza mzunguko wa biashara za awali.

Alisema hivi sasa halmashauri inakusanya Sh. bilioni 6.8 lakini chuo kita kapokamilika mapato yataongezeka kufikia Sh. bilioni tisa hadi 10.

# Waingiwa hofu wakisikia kisiwa kinabinafsishwa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAJASIRIAMALI na wafanyabiashara wadogo katika Kisiwa cha Kwale mkoani Mjini Magharib Unguja wameingiwa na wasiwasi wa kupoteza ajira zao, baada ya uwepo wa taarifa kuwa kisiwa hicho amepewa mwekezaji.

Wakizungumza na waandishi wa habari wajasiriamali hao walisema bado hawajapewa taarifa rasmi za kubinafsishwa kwa kisiwa hicho.

Mussa Muhamed Adam, alisema zaidi ya vijana 200 wamejiajiri katika kisiwa hicho na wanategemea kupata kipato kwa ajili ya kuendesha maisha ya familia zao.

"Zipo taarifa ambazo hatuna uhakika nazo ya kwamba tayari serikali imeshampa mwekezaji kisiwa hiki ambacho tunafanya shughuli zetu miaka 20 iliyopita leo hii tunakwenda wapi," alisema Adam.

Alisema wananchi kutoka maeneo mbalimbali ya Zanzibar wanakitumia kisiwa hicho kwa ajili ya kuwanufaisha kiuchumi na kuondokana na hali ya utegemezi.

Alisema iwapo taarifa hizo za ukodishwaji zitakuwa kweli vijana zaidi ya 200 watakosa ajira kwa sababu mwekezaji anapowekeza anakuwa na masharti yake na haruhusu watu kuingia katika maeneo hayo.

Alisema kuwa uhusiano wao na serikali bado upo vizuri, wanalipa ada zinazostahiki ikiwamo leseni na tozo kwa mgeni anayekwenda katika kisiwa hicho.

Mjasiriamali mwingine, Bahati Issa Suleiman alisema kuwa ni mwaka wa 20 anafanya kazi katika kisiwa hicho kwa lengo la kujikwamua kiuchumi.

Alisema kisiwa hicho ni tegemezi kwao kiuchumi na iwapo kitakuwa kimekodishwa ndoa zao zitakuwa hatarini kuvunjika.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar, Saleh Saed Mohammed, alisema ni kweli kisiwa hicho kimepata mwekezaji kupitia kampuni ya Grst Holding na wakati wowote kazi ya kufanya uwekezaji katika kisiwa hicho zitafanyika kwa maendeleo ya taifa.

Alisema kisiwa hicho kimekodishwa kwa mkataba wa Dola za Marekani milioni 68, taratibu zote zimefuatwa.

Alisema fedha za ukodishwaji wa kisiwa hicho ni mara mbili zaidi zinazopatikana sasa hivi, hivyo wananchi wanatakiwa kuwa na subira, kwamba hatua hiyo itafungua nafasi za ajira kwa wananchi wa maeneo hayo.

Alisema kukodishwa kwa kisiwa hicho kunafikisha idadi ya visiwa 16 hadi sasa vilivyokodishwa Zanzibar na serikali kupata Dola za Marekani milioni 385.

# Wananchi toeni elimu utunzaji mazingira kwa watoto

**Na Mwandishi Wetu**

WANANCHI wametakiwa kuzingatia utoaji wa elimu kwa watoto na vijana shuleni kuhusu masuala ya utunzaji wa mazingira.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya ECCT, Lucky Michael, alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki wakati akitoka elimu ya urejelezaji taka kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Daniel Chongolo, ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha Siku ya Usafi wa Mazingira Duniani.

Lucky alisema kuna umuhimu kwa watoto hususani waliopo shuleni kupewa elimu hiyo itakayowasaidia kuwajengea kiakili na kifikra katika suala ya utunzaji mazingira tangu wakiwa na umri mdogo.

"Wakati huu ambao taifa letu tunaendelea kupiga hatua kubwa katika utunzaji wa mazingira, sisi kama jamii tuna kila sababu ya kukielimisha kizazi cha watoto wetu walioko shuleni ili kukiwezesha kutambua faida za mazingira wakiwa bado wadogo," alisema.

Ofisa Habari wa ECCT, Nyanzobe Makwaia alisema katika kuhakikisha wanatimiza majukumu yao ya utunzaji wa mazingira, mbali na utoaji wa elimu kwa watoto shuleni wamekuwa wakishiriki katika usafi wa mazingira ikiwamo maeneo ya fukwe za bahari.

Alisema Taasisi ya ECCT iliyonzishwa miaka minne iliyopita imekuwa ikishirikiana na serikali katika kutimiza malengo yake ya utunzaji mazingira ikiwa ni pamoja na upandaji wa miti katika maeneo mbalimbali ikiwamo sehemu za utoaji wa huduma za jamii.

Mwalimu wa Mazingira wa Shule ya Daniel Chongolo, Mwanahamis Mhando, alisema kwao jambo hilo lilikuwa ni takwa kubwa kutokana na upya wa shule yao.

Alisema kutokana na uchanga wa shule hiyo kwa kiasi walikuwa na uhitaji wa elimu ya utunzaji wa mazingira kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi.

Nao raia kutoka Korea, Min Jeong Lee na Minj Kim ambao wapo wapo nchini kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo kuhusu utunzaji wa mazingira kupitia ECCT, wameipongeza Tanzania kutokana na juhudi inazozichukua kuboresha mazingira.

# Makamu wa Rais ataja dhumuni kuanzishwa PSSN

**Na Mwandishi Wetu**

Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) imeanzisha Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (PSSN) ili kupunguza umaskini uliokithiri.

Alisema hayo wakati wa hafla ya uzinduzi wa tathmini ya mwisho ya kupima matokeo ya Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini kipindi cha pili (PSSN II ).

Alisema mpango huo unaotekelezwa ndani ya awamu ya tatu ya TASAF, unalenga kuziwezesha kaya zinazoishi katika umaskini kuongeza kipato, fursa na uwezo wa kugharamia mahitaji muhimu. Hemed alisema kaya za walengwa hupatiwa ruzuku ya msingi pamoja na mafunzo ya stadi za ujasiriamali na mbinu za kuunda vikundi endelevu vya kuwekeza katika shuguli za kiuchumi ikiwemo kilimo na biashara.

Aidha, alisema kaya za walengwa hunufaika na fursa za ajira za muda mfupi na kujipatia kipato kwa kushiriki katika miradi mbalimbali ya maendeleo katika jamii.

Hemed alisema kuanzia mwaka 2000 hadi Agosti mwaka huu serikali imezisaidia kaya za walengwa 1,450,000.

Hivyo, alizitaka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar na Ofisi ya Taifa ya Takwimu Tanzania kuhakikisha tathmini inayofanywa inatoa takwimu zenye ubora zitakazoonesha taswira halisi ya hali ilivyo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu, Ali Suleiman Mrembo, alisema serikali imeweka mazingira mazuri ya kuhakikisha mradi huo unafanyika kwa ustadi na uweledi.

Hivyo, aliwataka wakuu wa mikoa na wilaya masheha na wananchi kutoa ushirikiano wakati wa kufanyika kwa zoezi la tathmini ili kupata takwimu sahihi zitakazoiwezesha serikali kujipanga zaidi.

Mkurugenzi Mtendaji TASAF, Shedrack Mziray, alisema madhumuni ya kufanyika kwa tathmini hio ni kuangalia ni kwa kiwango gani serikali imeweza kuwasaidia wananchi kupitia uwekezaji ilioufanya katika mpango huo.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Zanzibar, Salum Kassim Ali, alisema utafiti huo unatarajiwa kufanyika katika mikoa 17 nchini.



Mkurugenzi wa Kitengo cha Mazingira ya Biashara Ofsi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Baraka Algaesha (kushoto), akimkabidhi Mwanzilishi wa Blazers Store, Anna Kipeja tuzo ya Wanawake 50 Vijana Wajasiriamali, wakati wa hafla ya utoaji tuzo hizo iliyofanyika Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# SMZ yaendelea kuwekeza miundombinu ya elimu

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

NAIBU Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Ali Abdulgulam Hussein, amesema Serikali ya Zanzibar inaendelea kuwekeza katika miundombinu ya elimu, ili kuwawezesha wanafunzi kusoma katika mazingira mazuri.

Alisema hayo wakati akifunga maonyesha ya shamrashamra za elimu bila ya malipo Kisonge.

Alisema mabadiliko ya mitaala ya elimu yanaendana na majengo bora ya shule na ndiyo maana serikali inaendelea kujenga shule za kisasa.

Alisema hivi sasa serikali imeamua kujenga shule za ghorofa na zingine kuzifanyia matengenezo ili kuwafanya wanafunzi kusoma katika mazingira yanayokwenda.

Alisema kabla ya Mapinduzi ya Zanzibar wanafunzi wengi hawakupata nafasi ya kusoma kama ilivyo sasa, hivyo wakati umefika kwa wanafunzi kuendelea kuchangamkia fursa za elimu ziliopo.

Alisema kuwa serikali imeamua kubadilisha mitaala yake ya elimu na kujenga vyuo vingi vya ufundi kwa kila wilaya ili kuwajenga vijana kiujuzi. Ofisa Mdhamini wa wizara hiyo Pemba, Mohammed Nassor Salum, alisema kufanyika kwa maonesho hayo ni moja ya ubunifu kwa wizara ili kuweka wazi kazi zao wanazozifanya.

Ofisa mradi wa Shirika la Room to Read, Maria Mkembae, alisema kuwa taasisi hiyo inashirikiana vyema na serikali zote katika kuboresha masuala ya elimu.

# Mikoa 17 kufanyiwa tathmini ya umaskini

**Na Faustine Feliciane,** ZANZIBAR



SERIKALI kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) inaratajia kufanya tathmini ya upimaji matokeo mpango huo katika mikoa 17.

Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Sulleiman Abdulla (pichani), alisema hayo jana visiwani hapa wakati akizindua tathmini ya mwisho ya kupima matokeo ya kipindi cha pili ya cha mpango wa kunusuru kaya maskini kwa mwaka 2024.

Alisema mikoa 14 ya Tanzania Bara na mikoa mitatu ya Zanzibar yenye shehia, vijiji na mitaa 434 itafikiwa kwa ajili ya kufanyiwa tathmini hiyo.

Abdulla alisema kati ya hiyo, vijiji na mitaa 376 ni kutoka Tanzania Bara na shehia 58 ni kutoka Zanzibar.

"Madhumuni ya tathmini hii ni kupima endapo mpango huu unafikia malengo yaliyokusudiwa ya kuondoa umaskini kwa kaya zilizoainishwa kuishi katika umaskini uliokithiri," alisema Abdullah.

Alisema tathmini kama hizo hufanyika katika nchi mbalimbali duniani zinazotekeleza mipango kama kupitia taasisi za fedha na maendeleo za kimataifa.

"Katika nchi yetu, mpango huu unahusisha mikakati zaidi ya mmoja katika utekelezaji ili kuhakikisha walengwa wanafaidika na kutoka katika hali ya umasikini haraka.

"Hivyo basi, ni matarajio yetu tathmini hii itaweza kutoa taswira halisi ya hali ilivyo na kuiwezesha serikali kuona ni eneo lipi tunafanya vizuri zaidi na eneo lipi linahitaji kuongeza mkazo," alisema.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), Salum Kassim Ali, alisema matokeo ya tathmini ya mwisho ndiyo yatakuwa msingi wa kufanya uamuzi wa kuboresha zaidi hali ya upatikanaji huduma za kijamii na kuweka mikakati zaidi ya kupunguza umaskini nchini.

Alisema: "Tathmini hii ni muhimu ili kufikia lengo la mpango huu, kama ilivyoelezwa kwa awamu hii mikoa 17 itahusika na tayari mafunzo yametolewa kwa wale watakaofanya tathmini hiyo."

# ITU: Usalama mtandaoni ni muhimu dunia ya sasa

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Shirika la Mawasiliano Duniani (ITU), Dorren Bogdan Martin, amesema usalama wa mtandaoni ni muhimu zaidi kuliko ilivyokuwa miaka ya nyuma kutokana na kasi ya ukuaji wa teknolojia.

Pia amesema katika zama za taarifa na uchumi wa kidijiti, ambapo kila kitu kutoka masuala ya kibenki hadi burudani hufanyika mtandaoni, ni lazima kujenga imani katika ulimwengu wa dijitali kwa kuwekeza katika hatua za usalama wa mtandao zenye nguvu.

"Kadri taifa linavyokwenda sambamba na mabadiliko ya kidijiti, kumekuwa na ongezeko kubwa la watumiaji wanaounganishwa mtandaoni, huduma salama za mawasiliano ni suala la msingi hasa katika kutengeneza mtandao ulio salama kwa wote," anasema kiongozi huyo kupitia taarifa yake iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana.

Ripoti ya Usalama Mtandaoni ya Mwaka 2024 iliyotolewa Septemba mwaka huu, inaonesha Tanzania inaongoza nchi za Afrika Mashariki na Kati kwa kuwa na viwango vya usimamizi vya juu vya usalama mitandaoni.

Ripoti hiyo pia inaonesha Tanzania iko katika viwango vya juu vya mfano katika ufanisi wa kusimamia nguzo tano za usalama mitandaoni zilizowekwa na ITU kuanzia mwaka 2015.

"Shirika kwa kutambua umuhimu wa kuwa na mtandao unaoaminika, jumuishi na salama kwa watumiaji, miundombinu, taarifa za binafsi na kukuza uchumi wa kidijiti unaofanikiwa na ulio imara, lilianzisha vigezo vyenye nguzo zinazotakiwa kufuatwa na kila nchi mwanachama ili kuwa na usimamizi mzuri wa usalama mtandaoni," anasema katika taarifa yake hiyo.

Nguzo tano zinazopimwa kwenye ripoti hiyo inayojulikana kama ITU GCIv5 -2024, kifupisho cha jina lake kwa lugha ya Kiingereza, ni hatua za kisheria na ujenzi wa uwezo katika masuala ya usalama mtandaoni.

Nyingine ni mipango na mikakati ya kiufundi, mfumo wa usimamizi na ushirikiano wa usalama mtandaoni.

Mafanikio ya Tanzania yalikuwa asilimia 100 kwenye nguzo ya sheria, mifumo ya usimamizi na ushirikiano na asilimia 99 kwenye nguzo ya ufundi na kujenga uwezo.

Mambo yalivyochangia kupaa kwa Tanzania kwenye GCI ya 2024 ni pamoja na kuwapo mkakati wa kitaifa wa usalama mtandaoni, sheria na kanuni za mamlaka ya serikali mtandao (e-GA) na Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi 2022.

Pia Sheria ya Makosa ya Kimtandao 2015, Kanuni za Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (CERT) za 2018 na maboresho yake ya 2023 na Timu ya Kitaifa ya Mwitikio wa Kukabiliana na Majanga ya Kompyuta (TZ-CERT), timu iliyomo ndani ya muundo wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), timu za kisekta (GSoC) ndani ya e-GA na TZ-FINCERT inayosimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania.

Anasema ushirikiano wa wadau ndani ya nchi, kikanda na kimataifa pia umechangia kwa kiasi kikubwa kuiwezesha Tanzania kufanikiwa katika mchakato huu.

Akihojiwa jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari, alisema azma ya taasisi yake kama mwanachama wa ITU kwa niaba ya taifa ni kuendeleza dhamira ya kitaifa katika masuala ya usalama na uimara wa mtandao nchini.

Alisema TCRA itaendelea kushirikiana na taasisi nyingine za wazawa, kikanda na kimataifa.

Ripoti ya GCI ilianza kutolewa mwaka 2015 na ITU, Taasisi ya Umoja wa Mataifa inayosimamia masuala ya mawasiliano.

## KUPOTEA KWA KADI YA TREKTA

**BATHOROMEO JAPHET PILLA** anatangaza kupotea kwa kadi ya **TREKTA** yenye usajili namba **T 587 BCM ,** CHASSIS NAMBA: **899475M** na ENGINE NAMBA: **212UA43306.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**PHQ/ARU/ARU/35269/2024**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 19551/ 2024**

**In the matter of the Estate of the late SIMON LUCIAN ALUTE of MISSION Within Dodoma Region.**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY BRUNO THEODORY NTUKEY**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn. 369 of 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 24 Day of 09, 2024
Presented for filling this 09 Day of 09, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA KINONDONI MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI.....307.... LA 2023**

**GOODLUCK .E. MMARI..........MUOMBAJI/WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**DR. HAROUN ALLY.....................MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

**DR. HAROUN ALLY**
**POPOTE ULIPO/MLIPO**

**GOODLUCK .E. MMARY** amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni ( Mwananyamala) shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 10/10/2024 saa 03:00 asubuhi/mchana mbele ya Mh J.W.SILLAS Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 18 mwezi 09/2024

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) KINONDONI

## KUPOTEA KWA CHETI



**HELIME OCTAVIAN MULEBO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2266-0002** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa **GEORGIOUS SECONDARY SCHOOL** mwaka 2013. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/UBU/202555/2024**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**

**Kituo cha JUMUISHI** **Mkoa DAR ES SALAAM**

**Usimamizi wa mirathi Na 1486/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU NANZIA JOHN KILANGO WA DAR ES SALAAM**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MARCO GERMANUS MWANJELE**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/ maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 03 mwezi 10 mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakama kukaguliwa .
Imetolewa leo tarehe 19 Mwezi 09 mwaka 2024

HAKIMU

## KUPOTEA KWA CHETI



**MCHELE M. JULIUS** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1353-0102** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ZAKIA MEGHJI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2009. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DOD/DOD/RB/424143/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MESHACK ELIONA NDOSI** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye usajili namba **MC 827 DRS.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:
**PHQ/ARU/ARU/24987/2024**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**SANLG WORLD WIDE INVESTMENT CO. LTD** anatangaza kupotea kwa kadi za pikipiki zenye namba za usajili **MC 158 DZQ, MC 197 EKR na MC 199 EKR.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi:
**PHQ/IRI/IRI/14290/2024.**

## HABARI KIMATAIFA

# Trump aingia mitini mdahalo na Kamala

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa zamani wa Marekani, Donald Trump, amesema hatashiriki katika mjadala wa pili wa televisheni dhidi ya mgombea wa Chama cha Democratic, Kamala Harris kabla ya uchaguzi wa urais wa Novemba mwaka huu.

Ilielezwa kuwa wakati Makamu wa Rais Kamala Harris, ambaye ni mgombea wa Democratic, katika kinyang'anyiro cha urais akikubali mwaliko wa mdahalo wa CNN uliotarajiwa kufanyika leo, mgombea mteule wa Republican Trump alikataa akisema kwamba umechelewa kwa kuwa upigaji kura tayari umeanza.

**Awali, baada ya mjadala wa Septemba 10, mwaka huu Trump alisema hakutakuwa na mijadala zaidi.**

Timu ya kampeni ya Harris ilisema kwamba kutokana na rais huyo wa zamani kudai kuwa alishinda mjadala wao wa awali huko Philadelphia mapema mwezi huu anapaswa kukubali kushiriki mdahalo huo wa pili.

Wakati hayo yakiendelea ilielezwa kuwa kura za maoni zilizopigwa baada ya mkutano huo zilipendekeza kuwa wengi wa watazamaji waliamini kuwa makamu wa rais alimshinda mpinzani wake.

Awali, baada ya mjadala wa Septemba 10, mwaka huu Trump alisema hakutakuwa na mijadala zaidi.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara huko Wilmington, North Carolina juzi, alisema alishinda katika mdahalo wa kwanza na kumfanya mpinzani wake kupoteza, huku akimshutumu Kamala kwa kutafuta duru nyingine ya pambano.

Mwenyekiti wa kambi ya kampeni ya Kamala Walz Jen Dillon, alisema kuwa Wamarekani wanastahili fursa nyingine ya kuona mjadala wa Kamala na Trump kabla ya uchaguzi wa Novemba.

"Itakuwa jambo lisilokuwa la kawaida katika historia ya kisasa kwa kuwa na mjadala mmoja tu wa uchaguzi mkuu, mijadala inatoa fursa ya kipekee kwa wapiga kura kuona wagombea bega kwa bega na kutathmini maono yao ya ushindani kwa Marekani," alisema.

Kupitia mtandao wa X, ambayo zamani ilikuwa Twitter, Kamala alisema amekubali mwaliko wa mjadala kwa furaha na anatumai Trump pia atashiriki. **BBC**

## UN yashtushwa na RSF kuishambulia Al Fasher

**KHARTOUM,** Sudan

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres (pichani chini), amesikitishwa na taarifa zinazokihusu kikosi hasimu cha Msaada wa Haraka (RFS) kulishambulia kikamilifu jiji la Sudan la Al Fasher.

Awali Msemaji wa Umoja wa Mataifa, Stephane Dujarric, alisema Jumamosi kwamba Guterres alionya ongezeko lolote zaidi linalotishia kueneza mzozo katika eneo lote la magharibi mwa Darfur.

Msemaji huyo alisema kiongozi wa umoja huo alitoa wito kwa Luteni Jenerali Mohamed Hamdan kuchukua hatua kwa kuwajibika na kuamuru mara moja kusitishwa kwa mashambulio.

"Ni jambo lisiloeleweka kwamba pande zinazozozana zimepuuza mara kwa mara wito wa kusitisha uhasama," alisema.

Maofisa wa Umoja wa Mataifa walionya kuwa ghasia zinazozidi kuwa mbaya karibu na Al Fasher zinatishia kuzusha mizozo kati ya jamii.

Mshauri wa usalama wa taifa wa Marekani Jake Sullivan alisema kwamba mzozo huo utakuwa kwenye ajenda wakati Rais Joe Biden atakapokutana na Rais wa Umoja wa Falme za Kiarabu Sheikh Mohammed bin Zayed Al Nahyan leo.

Ilielezwa kuwa Sudan na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) zimezozana katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kutokana na shutuma za serikali ya Sudan yenye mafungamano na jeshi kwamba UAE inaipa silaha na kuiunga mkono RSF.



"Tuna wasiwasi kuhusu nchi kadhaa na hatua wanazochukua kuendeleza badala ya kutatua mzozo," Sullivan alisema. **TRT**



Athari zilizosababishwa na shambulizi la Israel karibu na eneo la Beirut Mashariki ya Kati. **PICHA: MTANDAO**

# Israel yaendelea kusababisha vifo Gaza

**GAZA,** Palestina

WIZARA ya Afya ya Ukanda wa Gaza imesema takribani watu 22 wameuawa kwenye shambulizi la kombora la Israel lililoilenga shule moja kaskazini mwa ukanda huo.

Wizara hiyo inayosimamiwa na Kundi la Hamas ilitoa taarifa hiyo jana na kueleza kuwa shambulizi hilo kwenye shule ya Zeitoun iliyopo katika mji wa Gaza pia limewajeruhi watu wengine 30.

Awali Jeshi la Israel lilisema limeishambulia kamandi ya kundi la Hamas, wanayodai ilikuwa imefichwa kwenye jengo ambalo zamani lilikuwa linatumika kama shule.

"Kundi la kigaidi la Hamas linakiuka sheria ya kimataifa kwa kuendesha operesheni zake ndani ya miundombinu ya kiraia," ilisema taarifa ya jeshi la Israel.

Ilielezwa kuwa Jeshi la Israel kila wakati limekuwa likililaumu kundi la Hamas kwa kufanya shughuli zake kwenye maeneo ya kiraia ndani ya Ukanda wa Gaza, ikiwamo shule na vituo vya Umoja wa Mataifa (UN).

Katika hatua nyingine kundi la wanamgambo la Hezbollah la nchini Lebanon limesema kwamba limefyetua makombora mawili kuelekea kaskazini mwa Israel.

Taarifa hizo zimetolewa katika wakati jeshi la Israel likitangaza kufanya awamu mpya ya mashambulizi ya kuzilenga ngome za Hezbollah.

Kupitia taarifa ya Hezbollah, kundi hilo linaloungwa mkono na Iran lilisema limefyatua makombora aina ya Katyusha kuzilenga kambi za kijeshi za Israel ikiwa ni jibu kwa mashambulizi kwenye vijiji na makazi ya watu kusini mwa Lebanon.

Makabiliano hayo yanatokea siku moja baada ya Israel kufanya shambulizi lililomuua kamanda mwandamizi wa Hezbollah Ibrahim Aqil mjini Beirut. Na kwamba shambulizi hilo la hivi karibuni lilisababisha pia vifo vya watu wengine 30.

Katika taarifa ya kuthibitisha kifo cha Aqil, ambaye alikuwa akitafutwa na Marekani kwa kuhusika katika ulipuaji wa ubalozi wa Marekani mjini Beirut mwaka 1983, Hezbollah ilimsifu kama mmoja wa viongozi wake muhimu.

Awali, Julai mwaka huu shambulio la Israel mjini Beirut lilimuua Fuad Shukr, Mkuu wa Operesheni za kundi na mauaji ya sasa ya kamanda mwandamizi Ibrahim Aqil ambayo yaliongeza hofu ya kuzuka vita kamili kati ya Hezbollah na Israel.

Aidha, Ofisa Mkuu wa Umoja wa Mataifa anayehusika na masuala ya kisiasa Rosemary DiCarlo, alizihimiza nchi zote zilizo na ushawishi juu ya Israel na kundi la Hezbollah kutumia ushawishi huo kuzirai pande hizo hasimu kusitisha mvutano ili kuepusha kutanuka kwa mzozo katika eneo la Mashariki ya Kati.

Rosemary alitahadharisha kuwa iwapo vita kamili vitatokea kati ya Israel na Hezbollah huenda vikasababisha uharibifu mkubwa zaidi kuliko ule ulioshuhudiwa hadi sasa.

Alitoa rai hiyo kwa wajumbe wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa baada ya kulipuka kwa vifaa vya mawasiliano vya Hezbollah ambako watu 37 waliuawa na maelfu ya wengine kujeruhiwa.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Lebanon, Abdallah Bou Habib, aliilaumu Israel kwa kuhusika na hujuma hiyo na kuongeza kuwa hakuna mtu yoyote duniani aliye salama.

Balozi wa Israel katika Umoja wa Mataifa Danny Danon alisema nchi hiyo haina nia ya kuutanua mzozo katika eneo la Mashariki ya Kati lakini haitaruhusu kundi la Hezbollah kuendelea na uchokozi wake. **DW**

# SIMBA SC, DODOMA JIJI FC SASA KUPIGWA JAMHURI

**Na Adam Fungamwango**

MECHI ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Dodoma Jiji na Simba iliyokuwa inanukia kupigwa Uwanja wa Tanzanite Kwaraa, Babati, Septemba 29, mwaka huu, imerudishwa kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma, imeelezwa.

Mechi hiyo itapigwa Dodoma baada ya Bodi ya Ligi (TPLB), kuurejesha tena Uwanja wa Jamhuri Dodoma katika orodha ya viwanja vitakavyotumika kwa michezo ya Ligi Kuu baada ya kuridhishwa na matengenezo yaliyofanyika.

**Taarifa iliyotolewa jana mchana na Idara ya Habari na Mawasiliano ya Bodi ya Ligi, ilielez kuwa awali iliufungia kutokana na kutokidhi vigezo hali iliyosababisha kupoteza sifa zilizoainishwa kwenye kanuni na sheria za mpira wa miguu.**

Taarifa ilieleza imeufungulia kutokana na sehemu iliyosababishwa ufungiwe ambazo kwa sasa zimerekebishwa ni eneo la kuchezea, mabenchi ya ufundi, na uzio unaotengenisha mashabiki na eneo la kuchezea.

Kutokana na kuufungulia uwanja huo, timu ya Dodoma Jiji itanufaika na urejeo huo, kwani katika mchezo wake wa kwanza wa nyumbani dhidi ya Namungo, Septemba 12, mwaka huu, ulichezwa Uwanja wa Tanzanite Kwaraa, Babati mkoani Manyara, na kupata ushindi wa bao 1-0.

"Bodi ya Ligi inautaarifu umma kuwa michezo ya nyumbani ya Dodoma Jiji iliyopangwa kuchezwa baada ya Septemba 28, mwaka huu, itachezwa kwenye uwanja huo kama ilivyoainishwa kwenye ratiba mama ya Ligi Kuu.

Aidha, Bodi ya Ligi inazikumbusha klabu zote kuhakikisha zinaendelea kutunza miundombinu ya viwanja vyao katika kipindi chote cha msimu kwani kushindwa kufanya hivyo kutashusha ubora wa uwanja na kusababisha viondolewe kwenye orodha ya vinavyotumika katika michezo ya ligi," ilisema taarifa hiyo.

## *Mtibwa yaanza Championship kwa hasira*

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Mtibwa Sugar imeanza Ligi ya Championship kwa hasira, baada ya kuichapa Green Warriors mabao 2-0 katika mchezo wa ufunguzi uliopigwa juzi, Uwanja wa Manungu Complex, Turiani mkoani Morogoro.

Mabao ya Mtibwa ambayo ilishuka daraja kutoka Ligi Kuu msimu uliomalizika, yalifungwa na Raizin Hafidh, dakika ya 35 na 70.

Ushindi huo umeifanya timu hiyo kuwa na mwanzo mzuri wa azma yao ya kutaka kurejea Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, Mbeya City ililazimishwa sare ya mabao 2-2 dhidi ya Bigman FC, ambayo zamani ilikuwa ikiitwa Mwadui FC.

Mabao ya wenyeji yalifungwa na Malack Joseph na Elius Ambokile, huku ya Bigman yakipachikwa wavuni na beki wa pembeni wa zamani wa Simba, Salum Kanoni na Omari Kisaga.

Katika michezo mingine, Songea United, ikiwa nyumbani, Uwanja wa Majimaji, iliichapa Mbeya kwanza mabao 2-1, Geita Gold, timu nyingine iliyoshuka daraja msimu uliopita, ililazimishwa suluhu nyumbani, Uwanja wa Nyankumbu, Geita, dhidi ya TMA, na Cosmopolitan, ikiwa Uwanja wa Jamhuri Morogoro, ililazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya African Sports.

Ligi hiyo yenye timu 16, imeanza rasmi kwa ajili ya kusaka timu mbili zinatazomaliza nafasi ya kwanza na ya pili, zitakazopanda moja kwa moja Ligi Kuu Tanzania Bara, huku ya tatu na nne hatima yao ya kupanda ikitegemea matokeo mazuri zitakapocheza mechi za 'play off.'



Watoto; Hamadi Ali (kushoto) na Amani Hassan, wakiwania mpira wakati walipokuwa wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Kopunovic avurugwa sare za Pamba Jiji

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuruhusu mabao mawili kipindi cha pili na kusababisha timu yake kutoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Mashujaa FC hapo juzi, Kocha Mkuu wa Pamba Jiji, Goran Kopunovic (pichani), ameonekana kuvurugwa, akisema labda yeye si mtu sahihi kwenye timu hiyo.

Ikiwa inaongoza mabao 2-0 mpaka dakika ya 74 kwa mabao ya Saleh Abdullah na John Nakibinge, yalirudishwa yote dakika ya 75 na 82, yakitiwa kwenye kamba na David Ulomi, hivyo kumfanya kocha huyo awashukie wachezaji wake kuwa walicheza kivivu baada ya kupata mabao mawili.

"Ni mbaya sana, baada ya kipindi cha kwanza bora kabisa tukafunga mabao mawili, kipindi cha pili mwanzoni tu tulipata nafasi ya kufunga mabao na kuimaliza kabisa mechi, badala yake tukaruhusu kirahisi mabao mawili, sielewi, nimehuzunika sana, hapa nilipo hata sielewi nifanye nini," alisema kocha huyo raia wa Serbia, akionekana kukata tamaa.

Alisema kila siku huwa anaongea na wachezaji wake, huku akifanya kazi kubwa ya kuwaelekeza nini cha kufanya, lakini wakiingia uwanjani wanafanya wanavyotaka wao.



"Kila siku nafanya kazi kubwa, naongea na wachezaji wangu, mabao 2-0 ni matokeo mazuri sana ya kupata ushindi katika soka duniani kote, sasa kama unashinda mabao mawili, halafu mnaanza kucheza kivivu na timu ambayo ina uzoefu kwenye ligi unategemea nini? Labda mimi si mtu sahihi kwenye timu hii," alilalamika.

Ulikuwa ni mchezo wa tano kwa Pamba Jiji kwenye Ligi Kuu na haijashinda mchezo wowote ule mpaka sasa, ikitoka sare nne na kupoteza mmoja.

Naye Kocha wa Mashujaa FC, Mohamed Abdallah 'Bares', alisema anashukuru kwa walichokipata licha ya kwamba walihitaji ushindi kwenye mchezo huo uliopigwa Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

"Sare ugenini si mbaya, tulikuwa tupoteze, nikafanya mabadiliko nikamwingiza Ulomi aliyefunga mawili, nadhani mechi ilikuwa inamhitaji," alisema.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### DAVIES, BAYERN BASI TENA

KLABU ya Bayern Munich imekata tamaa ya kurefusha mkataba wa Alphonso Davies mwishoni mwa msimu huu, huku Real Madrid wakimtaka beki huyo wa Canada mwenye umri wa miaka 23. ***(Relevo)***

#### TOMIYASU AVUTIA INTER

MLINZI wa Arsenal na Japan, Takehiro Tomiyasu, 25, amezivutia Napoli na Inter Milan. ***(Calciomercato)***

#### FONSECA HANA HOFU

KOCHA wa AC Milan, Paulo Fonseca, ambaye timu yake ilicheza na wapinzani wao, Inter Milan jana Jumapili, anasema hafikirii juu ya uvumi kuhusu mustakabali wake baada ya timu yake kuanza vibaya msimu huu. ***(Football Italia)***

#### LIVERPOOL KWA ZUBIMENDI

KOCHA wa Liverpool, Arne Slot, amesema klabu hiyo "imesonga mbele" kutokana na kushindwa kumsajili kiungo wa kati wa Hispania, Martin Zubimendi, 25, kutoka Real Sociedad msimu wa majira ya joto. ***(Mirror)***

#### DIAZ MKATABA MPYA

LIVERPOOL inaendelea na mazungumzo ya mkataba mpya kwa winga wa Colombia, Luis Diaz, 27, licha ya kukatishwa tamaa na wawakilishi wa mchezaji huyo katika kipindi cha majira ya joto. ***(Teamtalk)***

#### GARCIA HABABAISHWI

GOLIKIPA wa Espanyol, Joan Garcia, 23, amesema hakubabaishwa na nia ya Arsenal katika msimu wa majira ya joto, ingawa 'Washikabunduki' hao wanaweza kumnunua Mhispania huyo katika dirisha la uhamisho la Januari. ***(Mirror)***

#### PSG BADO NA MBAPPE

KLABU ya Paris St-Germain imekata rufaa dhidi ya uamuzi ambao utawalazimu kumlipa mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe, 25, ambaye alihamia Real Madrid msimu huu wa majira ya joto, pauni milioni 46 ambazo zimezuiliwa kama mshahara wake na marupurupu kutokana na muda aliohudumu katika klabu hiyo. ***(Athletic)***

#### XAVI ANA OFA KIBAO

KOCHA wa zamani wa Barcelona, Xavi, amesema amepokea ofa za kuvutia lakini bado hayuko tayari kurejea kwenye usimamizi wa soka kwa sasa. ***(Revelo)***


#### MITCHELL KUFUTWA KAZI

NEWCASTLE United itamfuta kazi Mkurugenzi wa Michezo, Paul Mitchell, kabla ya kufikiria kuachana na kocha, Eddie Howe iwapo mvutano kati ya wawili hao utaendelea. ***(Football Insider)***

#### DIBLING AVUTIWA NA UTD

KLABU ya Manchester United inamvutiwa na winga wa Southampton mwenye umri wa miaka 18, Tyler Dibling, lakini klabu hiyo ya Pwani ya Kusini inapanga kuongeza mkataba wake. ***(GiveMeSport)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ARSENAL KUTOMWACHIA GABRIEL KUTUA MADRID

### Pia PSG na Bayern zinahitaji huduma yake, zote kugonga mwamba kwani sasa inataka...

**LONDON,** England

ARSENAL inamwona beki wa kati Gabriel Magalhaes kama sehemu muhimu ya mustakabali wao na hatimaye watatafuta kumwongezea mkataba Mbrazili huyo, ripoti imefichua.

**Gabriel na beki wa kati, William Saliba, wote wamefurahia misimu miwili bora katika ngazi ya klabu.**

Mchezaji huyo hivi majuzi alijikuta akihusishwa na uhamisho na ripoti zinadai Real Madrid, Paris Saint-Germain na Bayern Munich zimeonesha nia ya kumnunua Gabriel, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 akidaiwa kuwa shabaha ya bei nafuu kuliko Saliba kwa vigogo wa Ulaya.

Ingawa nia ya watatu hao kwa Gabriel haishangazi kutokana na kiwango chake cha kustaajabisha, Fabrizio Romano anabainisha kuwa Arsenal hawajafikiria juu ya wazo la kuachana na Mbrazili huyo.

Mkataba wake utaendelea hadi 2027 na hadi sasa, hakuna maendeleo yoyote ya kuongezwa, ingawa hiyo ni kwa sababu Arsenal bado haijachukua hatua rasmi ya kumfunga Gabriel - jambo ambalo linawezekana kutokea katika siku za usoni.

Arsenal bado wanamwona Gabriel kama sehemu muhimu ya sasa na siku zijazo, na walionesha kujitolea kwao kwa kukataa ofa kutoka Saudi Arabia msimu uliopita wa majira ya joto.

Gabriel amekiri kwamba ilibidi ashawishike kubaki Arsenal na kocha Mikel Arteta, baada ya kupoteza nafasi yake kwenye kikosi cha kwanza kuanzia msimu wa 2023/24.

# TEN HAG AWAJIA JUU WACHAMBUZI KUHUSU RASHFORD



**LONDON,** England

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag, amewajibu wachambuzi kuhusu uvumi kwamba uamuzi wake wa kumweka benchi Marcus Rashford dhidi ya Crystal Palace Jumamosi haukuwa wa msingi isipokuwa "mzunguko" wa kawaida.

United waliondoka pale Selhurst Park wakiwa na pointi moja pekee kutokana na sare ya bila kufungana, licha ya kutawala kipindi cha kwanza, ambapo walipoteza nafasi nyingi za kuongoza.

Wito wa Ten Hag wa kumwacha Rashford kwenye benchi ulikuja kwa mshangao baada ya fowadi huyo kuifungia United bao lake la kwanza tangu Machi katika ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Southampton wikendi iliyopita na kufuatiwa na kufunga mara mbili katika ushindi wa 7-0 dhidi ya Barnsley Jumanne.

Alejandro Garnacho, ambaye alichukua nafasi ya Rashford kama badiliko pekee kutoka wikendi iliyopita, alishindwa kutumia nafasi mbili za wazi.

Wakati wote huo, Rashford alioneshwa mara kwa mara akiwa ameketi kwenye benchi na kamera za televisheni.

Mchambuzi wa Sky Sports, Jamie Redknapp, alipendekeza kabla ya mchezo kwamba kuna jambo linaweza kuwa limetokea kati ya Rashford na Ten Hag, lakini kocha huyo alijibu wasiwasi huo.

"Nimesikia uvumi tayari kutoka kwa wachambuzi. Ni wazimu, kama mtu hauko sawa unapoleta uvumi kama huo wakati haujui," alisema Ten Hag.

"Ilikuwa ni mzunguko tu. Nina furaha sana na Marcus katika kila kitu anachofanya."

Sare ya Jumamosi inamaanisha United itamaliza wikendi katika nusu ya mwisho ya msimamo ikiwa na alama saba baada ya mechi tano.

Watamenyana na FC Twente katika Ligi ya Europa Jumatano kabla ya mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Tottenham Jumapili wiki hii.

# Enrique: PSG haimpi shinikizo Dembele

**PARIS,** Ufaransa

KOCHA wa Paris Saint-Germain, Luis Enrique, amekuwa mwangalifu kuhusu kudokeza Ousmane Dembele kama mfungaji bora wa timu yake, akisema inaweza kuwa hatari kwa timu yake.

Bao la Dembele la kipindi cha pili katika sare ya 1-1 Jumamosi dhidi ya Reims liliisaidia PSG kuendeleza mwendo wao wa kutopoteza kwenye Ligue 1 na kumweka machoni pake kama mshambuliaji anayeongoza kuziba pengo la Kylian Mbappe aliyetimkia Real Madrid.

Hata hivyo, pamoja na kumsifia winga huyo mwenye umri wa miaka 27, ambaye msimu huu amefunga mabao manne na kutoa pasi mbili za mabao, kocha huyo aliitaka timu hiyo kwa ujumla kuimarika ili kutoweka presha kwa mchezaji mmoja pekee.

"Hatutafuti mfungaji wa bao, kwa sababu ukimpa presha Dembele halafu asifunge mabao unayotaka afunge, tutaanza na matatizo," alisema kocha huyo akiwaambia waandishi wa habari.

"Tunachotaka ni timu kushinda. Nani anafunga? Sijali. Acha mtu anayevaa jezi ya PSG afunge. Hakuna presha kwa mchezaji mmoja pekee. Timu nzima inabidi iendelee kuimarika," aliongeza.

PSG iliwasili Reims ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa dakika za lala salama dhidi ya Girona ya Hispania kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini ilitatizika kupata mdundo wao kutokana na kukosekana kwa wachezaji majeruhi kama vile mshambuliaji Marco Asensio na kipa Gianluigi Donnarumma.

"Tulijua tangu mwanzo kwamba ulikuwa mchezo mgumu sana. Walicheza vizuri sana, wana nguvu sana kimwili na walikuwa wazuri kwenye mpira," aliongeza kocha huyo.

Hata hivyo, Enrique alikuwa na imani kwamba mbinu ya timu yake ya kubadilisha nafasi ingewapa faida katika michezo ijayo, watakapoikaribisha Stade Rennais Ijumaa kabla ya kumenyana na Arsenal katika Ligi ya Mabingwa Ulaya siku nne baadaye.

# Ancelotti: Real Madrid inarudi kwenye ubora wake

**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti amesema timu yake inaimarika "kidogo kidogo" baada ya ushindi wao wa mabao 4-1 dhidi ya Espanyol kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Jumamosi.

Madrid walishindwa kufunga katika kipindi cha kwanza pale Santiago Bernabeu - wamefunga bao moja pekee la kipindi cha kwanza msimu mzima - na wakawa nyuma kwa bao la kujifunga la Thibaut Courtois. Kuanzishwa kwa Vinicius Junior - ambaye alipumzishwa mwanzoni - kulibadilisha mchezo, kwani mabao kutoka kwa Dani Carvajal, Rodrygo, Vinicius na Kylian Mbappe yaliipa Madrid pointi zote tatu.

"Nilidhani ulikuwa mchezo mzuri, tuliitikia vema baada ya bao la Espanyol," alisema Ancelotti katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi.

"Tulicheza vizuri zaidi, kwa mdundo zaidi, tulipata nafasi nyingi zaidi. "Tulicheza kwa kasi, tukisonga mpira kwa kasi zaidi, kwa mwendo mzuri zaidi ... uhamaji wetu ni silaha muhimu sana. Bao la tatu lilikuwa la kustaajabisha, shambulizi la kustaajabisha. Hatua kwa hatua tunarejea kwenye ubora wetu."

Madrid hawajawa na kiwango kizuri msimu huu, lakini hawajafungwa na kushinda mara nne na sare mbili kwenye LaLiga, na sasa wamecheza jumla ya michezo 38 ya ligi bila kushindwa.

Kumekuwa na tofauti kubwa kati ya maonesho yao ya kipindi cha kwanza na cha pili, huku mabao 17 kati ya 18 katika mashindano yote yakipatikana baada ya muda wa mapumziko.

"Tulizungumza kuhusu hilo na wachezaji kabla ya mchezo, ili kuona kama tunaweza kubadilisha hali hiyo, na hatukuweza," alisema Ancelotti.

"Mechi thelathini na nane bila kupoteza inaonesha timu imefanya vizuri sana."

Ancelotti alipuuzia mbali wasiwasi wake kuhusu kiungo wa kati Jude Bellingham - ambaye alihitaji matibabu kwenye bega lake baada ya kuanguka vibaya, akisema "haionekani kuwa na wasiwasi wowote."



HABARI MICHEZO

## Simba yatinga makundi ilipozoea

INATOKA UK. 24

wanasukumizwa nje ya michuano hiyo.

Ni kipindi ambacho kasi iliongezeka zaidi kuliko cha kwanza, huku Simba ikionekana kucheza nyuma ya mpira kwa muda mwingi wa mchezo.

Matukio ya kukumbukwa zaidi yalianza kutokea dakika moja kabla ya mechi kumalizika, wakati Al Ahli Tripoli walipokuwa wamehamia langoni mwa Simba, ambapo Mabululu aliachia mkwaju mkali ulioonekana unakwenda kutinga wavuni, lakini kwa ustadi wa kipa Camara, aliruka juu kama nyani na kuupangua mpira ukawa kona.

Kona hiyo ndiyo iliyokuwa kaburi lao, kwani wakati wanashambulia, Simba iliunasa na kufanya shambulizi la ghafla, kwa mpira mrefu ambao uliomkuta Balua, aliyekuwa ameingia kipindi cha pili, akakokota mpira kwa umbali mrefu, akawahadaa mabeki na kipa Ayman, kabla ya kuujaza wavuni kwa mguu wa kushoto.

## Gamondi: Hakuna wa kumwogopa

INATOKA UK. 24

timu kama Al Ahly, CR Belouizdad na bado tulifanikiwa kusonga mbele kuingia hatua ya robo fainali, sina hofu ya kukutana na timu yoyote," alisema Gamondi.

Katika hatua nyingine, Gamondi amewashukuru mashabiki wa klabu hiyo kwa namna walivyoisapoti timu yao kwenye hatua iliyopita.

"Ni jambo la kujivunia, ushindi huu umechangiwa na mashabiki wa timu hii, wamekuwa karibu na timu yao kila inapokwenda, kazi yetu ni kuhakikisha tunawapa furaha siku zote," alisema Gamondi.

**SINA TATIZO NA DUBE**

Kwa mara nyingine Gamondi amesema kukosa magoli kwa mshambuliaji wake, Prince Dube, ni jambo la kawaida kwenye mpira na anaamini atarejea kwenye ubora wake siku chache zijazo.

Dube juzi aliingia kipindi cha pili ambapo alipoteza nafasi kadhaa za kufunga kwenye mchezo huo walioibuka na ushindi wa mabao 6-0.

"Kama mnakumbuka Dube alikuwa hajacheza kwa muda mrefu wakati alipokuwa na mgogoro na klabu yake ya awali, kukosa magoli ni jambo la kawaida sana kwenye mpira, nimekuwa nikimwambia asiuzunike, taratibu atarejea kwenye makali yake, ni mshambuliaji mzuri na mwenye uwezo mkubwa," alisema Gamondi.

# 'WAMSHUKURU RAIS SAMIA KWA MOYO WAKE, AWAPA MIL. 85/-'

**Na Mwandishi Wetu,** Zanzibar

KLABU ya Yanga, imeendelea kutembelea upepo mzuri wa kuvuna mamilioni ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, baada ya juzi usiku visiwani Zanzibar, kuifunga timu ya CBE ya nchini Ethiopia mabao 6-0, hivyo wawakilishi hao wa Tanzania kuvuna Sh. milioni 30 za rais, kama sehemu ya motisha ya ushindi wao.

Kwa ushindi huo, Yanga imefanikiwa kufuzu hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu wa 2024/2025, ikiwa ni mwendelezo mzuri katika michuano ya Kimataifa kwa Yanga, ambapo pia kwenye mchezo wa kwanza uliochezwa Ethiopia, waliibuka na ushindi wa bao 1-0, hivyo kuvuna Sh. milioni tano 'Bao la Mama'.

> **Tangu Rais Samia aanzishe motisha wa Bao la Mama, Yanga wameonesha shauku kubwa ya kupata fedha hizo, ambapo kwa msimu huu tu tayari wamevuna Sh. milioni 85.**

Katika raundi ya awali, Yanga ilishinda mabao 4-0 dhidi ya Vita'O na marudiano ikaibuka na ushindi wa mabao 5-0, hivyo kujikusanyia jumla ya Sh. milioni 50 kabla ya kuvuna Sh. milioni 35 kwa ushindi wa jumla wa mabao 7-0 walioupata dhidi ya CBE.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa fedha hizo, Rais wa Yanga, Engineer Heris Said, alisema motisha wa Rais Samia unachangia kwa kiasi kikubwa timu yao kupata mafanikio makubwa katika michuano ya kimataifa.

Alisema tangu Rais Samia aanze kuonesha upendo kwa klabu za Tanzania, timu yao imekuwa ikitumia mwanya huo kuhakikisha kwamba wanatamba katika michuano ya kimataifa, wakiamini kuwa Bao la Mama ni maalum kwa kuwapa wachezaji wao moyo wa kufia uwanjani kama sehemu ya kukuza mchezo wa mpira wa miguu nchini Tanzania.

"Upendo huu ni mkubwa kwa rais wetu, hivyo tunamshukuru Mama Samia kwa kutuweka pazuri ndani na nje ya nchi, ndio maana tunashinda kwa magoli mengi uwanjani kwa sababu wachezaji wanafahamu shauku ya rais wetu ni kuona timu inashinda na kupata mafanikio makubwa.

"Hata ukiangalia wachezaji wanapokuwa uwanjani, utagundua nguvu zao nyingi zinachagizwa pia na mamilioni ya Rais Samia, kwetu Yanga tunamshukuru kwa kuonyesha upendo dhidi ya timu yetu," alisema Hersi.




Stephane Aziz akiungana na Price Dube (katikati), sambamba na Kennedy Musonda, kushangilia baada ya kuifungia timu yake moja kati ya mabao matatu (hat-trick), wakati wakishinda 6-0 dhidi ya CBE ya Ethiopia kwenye mechi ya marudiano ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa New Amaan Complex visiwani Zanzibar jana. **MPIGAPICHA WETU**

# Job: Fedha za Mama zinatupandisha morali

**Na Faustine Feliciane,** ZANZIBAR

BEKI wa kati wa Klabu ya Yanga, Dikson Job, amesema ushindi mkubwa wanaoupata kwenye michuano ya kimataifa unachangiwa kwa kiasi kikubwa na ahadi ya fedha za Rais Samia Suluhu Hassan anazozitoa kwa kila bao wanalofunga.

Job ambaye kwenye mchezo wa juzi dhidi ya CBE ya Ethiopia alikuwa nahodha wa timu hiyo, alisema, kila wakati wamekuwa wakihamasishana wachezaji kupambana uwanjani kwa sababu ya fedha hizo na kuendelea kuwapa furaha Wanayanga.

"Ni kweli kabisa ushindi huu na hata mechi iliyopita kwenye michuano hii, pesa za mama yetu zimekuwa zikitupa hamasa sana, huwa zikitolewa tunagawana wachezaji wenyewe, kwa hiyo kila mmoja huwa anajitolea kuhakikisha tunapata ushindi mkubwa tupate pesa nyingi," alisema Job.

Akizungumzia mchezo huo wa juzi, Job alisema ulikuwa mgumu kutokana na aina ya uchezaji wa wapinzani wao.

"Kipindi cha kwanza wapinzani wetu walikuwa wengi sana kwenye eneo lao la nyuma, walitoa upinzani wa namna ya kufika golini kwao na ndio maana uliona hatukupata magoli mengi, lakini tulipoenda mapumziko kocha alitupa maelekezo na tuliporejea tulianza kwa kasi na kufanikiwa kupata bao la mapema kipindi cha pili," alisema Job.

Alisema baada ya bao hilo la pili waliendelea kuimarika kimchezo na kuwabana wapinzani wao kwenye eneo lao na kufanikiwa kupata mabao sita.

"Kwa sasa tumemaliza hatua hii, tunaelekea hatua ya makundi kocha wetu anajua nini tunatakiwa kufanya kuweza kufanya vizuri zaidi ya msimu uliopita," alisema.

# Michezo

Jumatatu Septemba 23, 2024

Nipashe




Arsenal kutomwachia Gabriel UKURASA 21

# SIMBA SC YATINGA MAKUNDI ILIPOZOEA

## Ni baada ya Kibu kufungua njia, Ateba akapokea kisha Balua akahitimisha kilio kwa Al Ahli Tripoli, sasa...

**Na Adam Fungamwango**

WAWAKILISHI wa Tanzania katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, Simba, wamefanikiwa kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo mara ya pili kwa kipindi cha misimu minne baada ya kuiadhibu Al Ahli Tripoli mabao 3-1 katika mchezo mkali na mgumu uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Yalikuwa ni mabao ya Kibu Denis, Leonel Ateba na Edwin Balua yaliyoipeleka Simba hatua hiyo ambapo sasa itasubiri droo inatayochezwa baadaye mwezi ujao.**

Ulikuwa ni mchezo wa mkondo wa pili baada ya ule wa kwanza wa raundi ya kwanza Jumapili iliyopita kwenye Uwanja wa Juni 11, nchini Libya, timu hizo kutoka suluhu.

Hii inakuwa ni mara ya nane kwa Simba kucheza ligi za kimataifa, tangu zilipoanza kuchezwa kwa mtindo wa makundi, Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho.

Pia ni mara ya tatu mfululizo kutinga makundi ya mechi za kimataifa kwani misimu miwili iliyopita ilicheza hatua kama hizo za Ligi ya Mabingwa Afrika.

Haikuwa rahisi kwa Simba kutinga hatua hiyo, kwani ilipigana machozi, jasho na damu kuweza kupata mabao hayo, kutokana na kutangulia kufungwa.

Simba ilianza kugonga hodi langoni mwa wapinzani wao dakika ya pili tu, baada ya Shomari Kapombe kuambaa na mpira kwenye wingi ya kulia, lakini krosi aliyopiga ilishindwa kuzuiwa na Joshua Mutale na kusababisha mabeki waokoe.

Dakika nne baadaye ilirejea tena, safari hii krosi ya Mohamed Hussein 'Tshabalala', ilikwenda langoni, lakini Ateba aliyekuwa katika nafasi nzuri, akateleza na kuanguka, akiwapa fursa mabeki wa Al Ahli kuuokoa mpira huo.



Kiungo mshambuliaji wa Simba, Kibu Denis, akimtoka beki wa kati wa Al Ahli Tripoli, Ahmed El Trbi, kwenye mechi ya marudiano ya hatua ya kwanza ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam jana na kumalizika kwa wenyeji kushinda mabao 3-1. **NA MPIGA PICHA WETU**

Kosa lililofanywa na Tshabalala dakika ya 10 nusura liwapatie bao Al Ahli, kwani alirudisha fyongo langoni mpira kwa kichwa, lakini ulikuwa mfupi, shukrani kwa kipa Moussa Camara aliyeuwahi kabla ya straika hatari, Agostinho Cristovao Paciencia maarufu kama Mabululu hajaifikia.

Mabululu aliwashtua mashabiki wa Simba dakika ya 17 kwa kuukwamisha mpira ndani ya wavu, akitumia uzembe wa mabeki wa timu hiyo kushindwa kuokoa mpira wa faulo iliyopigwa na Sunday Masoud.

Faulo hiyo ilipigwa kwenye wingi ya kushoto, ukarudishwa ndani na Mohamed El Munir, mabeki wa Simba wakazubaa, mpira ukawekwa ndani ya wavu.

Simba ingeweza kusawazisha bao dakika tatu baadaye kama si shuti la Joshua Mutale lisingemgonga mmoja wa mabeki wa timu hiyo na kutoka nje.

Kibu aliisawazishia Simba bao dakika ya 35, kwa 'kutambuka' kwa ustadi na kuunganisha mpira wa kichwa uliopigwa na Fondoh Che Malone.

Ulikuwa ni mpira wa adhabu uliopigwa na Jean Charles Ahoua ambao ulipigwa kichwa na beki huyo ukarejea ndani kabla ya kumkuta mfungaji ambaye aliukwamisha wavuni licha ya kipa Ayman Al Tihar kujitahidi kuokoa.

Sekunde chache kabla ya kwenda mapumziko, Ateba aliwainua vitini mashabiki wa Simba alipopachika bao la pili baada ya kupokea pasi ya kupenyezwa kutoka kwa Mutale.

Yalikuwa ni makosa ya mmoja wa mabeki wa Al Ahli Tripoli kurudisha mpira nyuma, ambao uliporwa na wachezaji wa Simba na kufanya shambulio lililozaa bao hilo.

Kipindi cha pili kilikuwa na presha zaidi kwa wachezaji, viongozi, benchi la ufundi na mashabiki wa Simba kwani walihitaji bao moja ambalo lingewaweka salama, lakini haikuwa hivyo mapema.

Kila mmoja alitambulia kuwa kama wapinzani wangepata sare yoyote ile, wawakilishi hao wa Tanzania walikuwa

INAENDELEA UKURASA 23

## Gamondi: Hakuna wa kumwogopa makundi

**Na Faustine Feliciane,** ZANZIBAR

BAADA ya kuiwezesha timu yake kufuzu hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema kwa sasa hakuna timu wanayoihofia kukutana nayo kwenye hatua hiyo.

Yanga juzi usiku ilitoa CBE ya Ethiopia kwa jumla ya mabao 7-1 baada ya kushinda 6-0 katika Uwanja wa New Amaan Complex visiwani Zanzibar, ushindi huo ukija wiki moja baada ya kutoa kipigo cha bao 1-0 ugenini.

Akizungumza juzi baada ya mchezo huo wa marudiano hatua ya kwanza ya michuano hiyo, Gamondi, alisema wanachokifanya ni kuwaheshimu wapinzani wao, lakini hakuna timu wanayoihofia.

Gamondi, alisema kufuzu kwa Yanga kwenye hatua hiyo ni jambo jema kwa nchi kwani inakuwa mwakilishi kwenye michuano hiyo mikubwa kwa ngazi za Klabu Afrika.

"Sasa tunasubiri droo ya makundi, tunashukuru tumeingia kwenye hatua hii kama yalivyokuwa malengo yetu, Yanga kwa sasa ni miongoni mwa timu kubwa Afrika, tuna kikosi kipana cha wachezaji wenye uwezo unaolingana, hatuiogopi au kuihofia timu yoyote kwenye hatua inayofuata, tupo tayari," alisema Gamondi.

Aidha, aliweka wazi kuwa analijua soka la Afrika na tayari amekushakutana na timu kubwa tangu akiwa anafundisha soka Afrika Kusini, hivyo hana cha kuhofia.



"Msimu uliopita tulipangwa kwenye kundi gumu na

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >